BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/ Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda/ Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na**

			Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**

31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**

54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 25 Mei, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuanza majadiliano hayo naomba sana niwaambie kwamba leo ni siku ya Ijumaa na tunatakiwa wizara hii tuimalize leo hii. Kwa maana hiyo, ikifika saa 6:00 tuhakikishe kwamba tumemaliza shughuli yetu hii ya leo. Nina wachangiaji 19. Sasa hapa ninaona tukubaliane kwamba na ninafikiria ndio sahihi kabisa, tukubaliane kwamba tuchangie ili aweze kupata kila mtu katika hao 19 tuchangie kwa dakika 5. Mambo mengi yameshazungumzwa, kwa hiyo ningeomba sana hiyo dakika 5 mtu azungumze yale ambayo anahisi ni muhimu zaidi. Nafahamu kwamba wengi wameandika mambo mengi wanataka kuyagusia, lakini nafikiria kwamba tayari mmeshayazungumza mengi, wengi waliopita wameyazungumza. Ningeomba tu watu wajipange kwa kutumia dakika 5 ili kila mmoja wetu aweze kupata nafasi ya kuchangia, laa wale ambao wanaona kwamba watashindwa kuzungumza kwa dakika 5 anaweza akapata dakika 5 halafu akaandika kwa maandishi akapeleka kwa Mhe. Waziri nayo pia inakubalika. Ahsanteni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami nikushukuru na nianze kuangalia dakika zangu 5 hizi na nitajaribu kuheshimu. Kwanza, nitoe shukrani zangu za dhati nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii, Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa busara zake, hekima zake, ujasiri wake, uzalendo wake na kubwa kuliko yote utulivu wake. Dkt. Mwinyihaji pongezi sana nakupa hizo wala hukuteteruka, wala hukupeperuka, umetoka mbele umekuja nyuma umekuwa mtulivu kweli kweli na Mwenyezi Mungu akuendeleze hivyo hivyo na fikra zako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini hakuomba uwaziri ameomba uwakilishi, huu uwaziri kazi ya ziada. Umetoa darasa kubwa sana Dkt. Mwinyihaji na Mwenyezi Mungu akujaalie hivi hivi kwa moyo wako. Nimeipenda sana tabia yako Dkt. Mwinyihaji, nimeipenda sana, sana kabisa, hukuteteruka, wala hukuyumba, wala hukuyavamia haya mambo. Nafikiri hakuna mtu aliyekukaribia humu umeongoza karibu wizara nne, hakuna katika waziri

ninaowatizama humu wa kukukaribia wewe umefanya kazi kubwa kipindi kilichopita na nyuma yake. Kwa hiyo, nikutakie kila la kheri, afya njema, lakini vile vile makamu wako katika kamati hii imepata viongozi maana yake watu wazima, busara nyingi ikiwa chini ya Makamu Mwenyekiti mmefanyakazi vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, hata Katibu wa kamati hii ni mtu mtulivu kweli kweli katulia sana, sitaki kutofautisha na kamati nyengine, lakini hii kamati moja nzito mmefanyakazi. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini hongera sana, tena sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitahitaji maelezo kidogo tu ingawa ndio pesa zimepungua kutoka 1.179 zimepelekwa katika ugatuzi niombe serikali na Waziri wa Fedha na Mipango sijui yupo hapa, nafikiri yupo, Waziri wa Fedha nikuombe sana kama Wizara ya Afya unavyowaingizia fedha asilimia 100 au *quarter* nzima na hii inahitaji hivyo, vyenginevyo tutawabebesha au msalaba uliokuwa sio wao. Mhe. Waziri nikuombe sana fedha, kazi ya Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoifanya yote itakuwa bure, tumeshuhudia kazi kubwa aliyoifanya katika wizara hii, maskuli ya kileo yamejengwa nilizungumza mimi katika wizara yake. Kama hakupewa asilimia angalau 90, 95 itakuwa kazi yote inayofanywa ada ya maskuli yanaondoshwa itakuwa bure bila ya fedha hawezi kufanya kitu.

Mhe. Naibu Spika, fedha ndio itakayowasaidia kuwainua vyenginevyo vyovyote tutawalaumu. Mheshimiwa nilikuwa niombe tena hapa nitakuja kuzuia fungu ni-*declare* kabisa. Nilikuwa naomba kuwepo na sehemu ya utumishi wa walimu tu kama itakuwa Wizara ya Utumishi au itakuwa Wizara ya Elimu, walimu hawa watakuwa wanasikitika pa kwenda hawana. Walimu wanafanya kazi nzito, kama itakuwa Wizara ya Utumishi ndio inayotoa Wizara ya Utumishi ina mambo mengi, lakini tena siingilii mamlaka ya Rais, hawa walimu watafanya kazi watachoka hawajui matatizo yao yatakwenda wapi. Niombe na hapa nitakuja kuzuia fungu nasema kabisa, lazima paundwe Tume ya Walimu matatizo yao yatakwenda wapi kama kitengo hichi kitakuwa Utumishi au Wizara ya Elimu. Vyenginevyo vyovyote itakuwa tunatwanga maji kwenye kinu kazi anayoifanya Mhe. Rais tunaiona na tuipongeze kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ninavyokisia kuna walimu watastaafu karibu hawapungui 300 au 400 kwa Unguja na Pemba waajiriwa wako wapi watakao-*cover* mapengo haya. Niombe hili zoezi mlizuie vyenginevyo kazi yote anayoifanya Mhe. Rais itakuwa bure. Kwa nini wasiongezwe mkataba, kuna wastaafu wangapi wanaongezwa mikataba. Hili niliombe sana, hasa walimu wa sayansi *specific* wanaotaka kustaafu wazuiwe vyenginevyo itakuwa ni mtihani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia ubora wa elimu nataka kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

1. Kuunda Tume ya Wataalamu kupitia ubora wa mfumo mzima wa elimu Unguja na Pemba hili ndilo litakalotusaidia vyenginevyo vyovyote kazi itakuwa bure.
2. Kuangalia matatizo ya walimu, walimu wanafanya kazi nzito wana matatizo hawajui wakaseme wapi.
3. Masaa ya wanafunzi wanayosoma yaangaliwe nayo nashauri.

4. *Syllabus* zote ziangaliwe hii ya Unguja na Pemba ndio yote moja Wizara ya Elimu iangaliwe ikoje. Leo pengine mtoto wa darasa la nne ndio anasomeshwa kizungu tofauti na skuli za *private* hili nashauri.

Mhe. Naibu Spika, kuna hii *"O" level* miaka 4, *"A" level* miaka 2. Nimalizie nitahitaji maelezo ya Skuli ya Mtule, Jimbo la Paje kwa nini inavuja ile skuli mpya imejengwa. Hivi sasa haikaliki kule nitahitaji maelezo inatoka Jimbo la Paje. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*
Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kabla ya kuchangia kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima, lakini pia niipongeze Kamati ya Elimu na Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Hata walipokuwa wanasoma majina nikasema kweli hii kamati imejaa watu wa hikma.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, waziri ambaye katika mawaziri wa serikali hii ya SMZ kati ya waziri ambaye namuamini yeye mmoja akiwemo. Sina wasi wasi nae kwa kuwa waziri huyu tuli-*oper* wakati wa ujana wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda moja kwa moja katika mchangio na sitokuwa na mambo mengi nitachangia kuhusu ruzuku na walimu nafupisha ili niwahi muda. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Rais kwa kufuta michango ambayo wazee wanatakiwa kuchangia katika skuli za sekondari. Nimpongeze kwa juhudi zake anazozifanya niwaombe sana watendaji na waziri kama akiwa msimamizi kuunga mkono jitihada hizi za Rais na wasimuangushe kwa sababu kama hizi fedha hazitokuwa zinafuatiliwa basi matatizo ya maskulini na walimu yatabaki kuwa pale pale, ruzuku imetolewa lakini fedha kwa kuwa ni ruzuku itakwenda watu watafanya wanavyotaka. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri na watendaji wake wawe wanafuatilia wasiwe watendaji wa kwenye meza wawe wanatoka kwenda kufuatilia. Najua waziri hawezi akapita kote lakini kama wasaidizi wake watamsaidia vizuri basi hizi ruzuku zitapunguza yale matatizo ya walimu na elimu nzima kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumzia kuhusu suala la ruzuku naomba niingie kwenye suala la matatizo ya walimu. *Speech* ya kamati imezungumza hapa kwamba walimu wana changamoto nyingi mno na wameziandika. Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka kuzungumza na walimu hapa pamoja na kwamba wana changamoto lakini na wao wajitahidi sana kutoa huduma kwa watoto. Kwa sababu ukisema usifanye kazi kwa kuwa una changamoto taifa hili tunalipotosha na kesho hatujui tutakuwa na taifa gani kama watoto wanaendelea kufeli kama wanavyoendelea kufeli hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana walimu wawe wazalendo, kuna mambo mengi wanajihusisha ambayo hayawahusu, wanajihusisha kwenye siasa, wanajihusisha kwenye mambo mengine ambayo hayawahusu, lakini wakitulia katika kazi zao na kufanya hii kazi basi na serikali nayo itatizama changamoto zao ili kuona kwamba wanatatuliwaje, lakini na wao *atleast* tuone ile *delivery* yao kwa watoto. Mhe. Naibu Spika, tunataraji kwamba baada ya hizi ruzuku kutoka mwakani matokeo ya watoto yata-*improve* na sio kama yalivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nimalize dakika 5 zimekwisha nina wasiwasi sana na naunga mkono mchango alioutoa Mhe. Panya Ali Abdalla kuhusu walimu ambao tuna-*import* kutoka Nigeria.

Mhe. Naibu Spika, msaada ndio msaada tusiwe kwamba tunaleta msaada baadae tukaja kujitafutia matatizo na walimu hawa kwa sababu wanakuja na wanakuja ku-*mingo* ama ku-*interfere* katika jamii yetu. Kwa hiyo, naomba sana serikali iwafuatilie wajue *background* yao huko wanakotoka lakini pia wawe *vetted* kabla ya kuwaingiza katika jamii yetu tusije tukatafuta matatizo mengine baadae. Nafahamu kwamba tuna *shortage* ya walimu wa sayansi lakini *we could import* hata kutoka Tanzania Bara wapo walimu na watu hawana ajira, kwa nini tukachukue nje badala ya ku-*import* kutoka Tanzania Bara ili tukadumisha Muungano wetu kwa zaidi. Mhe. Naibu Spika, sina mengi baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir, mchangiaji anayefuata kama nilivyosema ni Mhe. Mussa Foum Mussa, ajitayarishe Mhe. Shaib Said Ali.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kuchangia kidogo. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea hotuba yake hii ya bajeti pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote wa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo vile vile nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa msukumo mkubwa zaidi na kuliendeleza lengo la Rais wa Kwanza wa nchi hii, baada ya kusema kwamba kuondosha malipo yale ya elimu ya msingi na sekondari. Kwa hiyo, nadhani amejitahidi na anaendelea kujitahidi juu ya suala la elimu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niipongeze Kamati ya Ustawi wa Jamii nadhani wenzetu wamejitahidi sana na wametoa maelezo ya muangaza kuhusu habari ya elimu. Kwa hivyo, nadhani ni vyema na wao tukawapongeza. Baada hapo nitaanza kuchangia katika Programu ya kwanza ya Elimu ya Maandalizi na Msingi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake hapa ukurasa wa 7 ameeleza kwamba idara inasimamia Madrasa na Vyuo vya Qur-an pamoja na vituo 324 vya Tucheze na Tujifunze (TUTU). Nadhani Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo zuri lakini mimi nataka niwaulize tu kwamba hizi madrasa na vyuo vya qur-an wanavisaidia kwa njia gani. Hapa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze hasa kwa sababu kwanza mimi natoa maelezo kwamba walimu wetu wa vyuo vya qur-an ni wengi na wanajitahidi sana katika kuendeleza imani yetu ya dini ya kiisalam, lakini na wao hali zao ngumu. Sasa kama wizara au serikali je, hawa walimu wa qur-an mnawasaidia vipi katika hali hii kwa sababu hawa walimu wa TUTU wao nadhani angalau kuna sabuni wanayogaiwa. Lakini je, hawa walimu wa vyuo vya qur-an tunawaangalia vipi na wao wanajenga taifa na kwa muda mkubwa. Kwa hivyo nadhani ni vyema serikali na wao ikawaona.

Mhe. Naibu Spika, baada ya suala hilo vile vile nielezee kwamba na mimi katika jimbo langu ninazo skuli ambazo zina matatizo. Kwa mfano, tuna Skuli ya Msingi ya Kiwani Tasini hii juzi nilipokwenda kuitembelea katika kipindi hichi cha mvua kuna mabanda wameeleza humu katika

bajeti yao kwamba wametenga fungu la kufanya ukarabati kwa baadhi ya skuli. Naomba na hii Skuli ya Kiwani Tasini basi iangaliwe kwa sababu hivi sasa kukinyesha mvua watoto hawawezi wakapata pa kusomea kwa sababu banda lote linavuja. Na pale pale tuna ujenzi na umeshakuwa katika hali nzuri, basi kesho kutwa tunamalizia katika kufunga linta, tunakuombeni katika mabanda nayo myaweke katika ule ufadhili wenu wa kumalizia skuli.

Vile vile katika Skuli ya Shamiani Muambe nako kuna banda la mwanzo linatakiwa kufanyiwa ukarabati tumeanza kufanya lakini hali ngumu. Kwa hiyo, tunaiomba wizara na sehemu hii na wao wajitahidi kulimalizia lile banda la Skuli ya Shamiani Muambe kwa sababu liko katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, niende haraka haraka vile vile bado naelezea upungufu wa walimu katika Skuli ya Muambe. Kwanza niishukuru na niipongeze tena Kamati ya Ustawi wa Jamii katika skuli hii ya Muambe wameshafika.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nimeshalielezea katika bajeti zote tatu kwa sababu tokea umalizike uchaguzi bajeti hii ni ya tatu, na kila bajeti suala hili la upungufu walimu Skuli ya Muambe nalielezea. Wao wizara kama wizara wameshafika katika skuli hii na hili suala wameshaliona ni la kweli. Sasa kuna tatizo gani kwamba hili suala lisitekelezwe au lisipunguzwe.

Mhe. Naibu Spika, hili suala ni zito. Watoto wanakwenda mikondo mitatu, watoto wa msingi Muambe ni wengi. Katika mwaka 2017 tuliwaandikisha watoto 611, pale tukawa tuna upungufu wa walimu 30, mwaka huu tumeandikisha watoto 985. Tulikuwa na upungufu wa walimu 30 tu katika walimu walioajiriwa tumepata walimu 13.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika moja.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Haya. Kwa hivyo, si haba angalau tumepata kidogo. Lakini bado lilipokuja ongezeko la wanafunzi kuandikishwa 985 bado lile tatizo la walimu limezidi. Sasa nanalokuombeni hili suala tusilizungumze tena hapa, tunategemea sisi waheshimiwa tunapozungumza hapa lile suala lifuatiliwe na likionekana lina ukweli basi litekelezwe, huu ndio utaratibu. Lakini kila siku mtu atasema jambo hilo hilo, sio vizuri. Mhe. Naibu Spika, mimi sipendi hasa kupiga buti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nina mengi lakini niseme kwamba naipongeza Skuli yangu ya Muambe katika zile skuli tisa ambazo zinajengwa skuli za ghorofa na sisi tumepata si haba *Alhamdulillah* kwa hivyo nadhani tutapunguza tatizo hilo. Lakini naomba suala la upungufu wa walimu liangaliwe tena na tena. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Shaib Said Ali na ajitayarishe Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniona katika kuchangia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wizara ambayo wengi imetulea na wengi tumeifanyia kazi na mpaka sasa hivi bado tunaendelea kuifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nimpongeze Mhe. Waziri, watendaji wake wote, pamoja na walimu wote kwa sababu walimu wana kazi kubwa, wana juhudi kubwa na ndio maana wengi leo hapa tukasimama kuweza kusema haya tunayoyafahamu. Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba sisi walimu tumeingia humu kama katiba inavyojieleza, hatukuingia kwa mujibu kama tunavyotaka, tumeingia kikatiba humu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nije katika uchangiaji wangu niizungumze sera. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna sera ya 4, 6, 10, 12. Naomba Mhe. Waziri atuelezee kwa sababu hivi sasa kuna utaratibu kwamba wanafunzi wanapofika darasa la kumi wa mwaka jana wanaanza kufeli pale, na hii ndio sasa hivi wananchi wanaelewa hivyo.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri atuelezee, wanafunzi hawa wanaofika darasa la kumi wakafeli kwa sababu bado wanafunzi wale ni wadogo, wanawapa wazee mzigo mzito sana. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pale atuelezee wanafunzi wale hivi sasa wataendelea kufeli pale au ndio mpaka darasa la kumi na mbili wataendelea, awaelezee wananchi ili wasikie kwa sababu wengi wanaulizia ndio sasa watoto wetu wataanza kufeli darasa la kumi kama kawaida. Kwa sababu watoto ni wadogo na mzigo ni mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, hii sera ikiwa wanafunzi watafeli darasa la kumi pale, bado vijijini watoto ni wadogo sana. Mimi namuomba Mhe. Waziri hili suala atuelezee, wanafunzi wale watakaofeli darasa la kumi pale wataendelea mpaka darasa la kumi na mbili au ndio mwisho pale.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia suala la Vyuo vya Qur-an. Kwa vile na mimi ni mmoja muumini nazungumzia tena Vyuo vya Qur-an. Mhe. Naibu Spika, bado walimu wa qur-an wananyanyasika. Kunyanyasika kwa walimu wale ndio mpaka leo hii tukaona kwamba tuna shida gani Zanzibar mpaka haya majanga yote yakatuelemea namna hii. Majanga yale yametuelemea kwa sababu tumeidharau dini yetu ya kiislam. Moja katika kuidharau ni kuwadharau walimu wa masomo ya qur-an. Tumewadharau maana yake wananyanyasika, hawatambulikani. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri hili suala aliangalie kama limegatuliwa katika Serikali za Mitaa lijulikane na kama bado liko Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali lijulikane kuhusu hawa walimu wa Vyuo vya Qur-an.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika maandalizi ya elimu. Mheshimiwa siku zote elimu inaanzia katika maandalizi, lakini bado elimu hii ya hapa haijapangika vizuri na pale ndio msingi mbovu wa elimu unapoanzia. Kwanza majenzi mabovu, upungufu wa walimu, vifaa na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri anifahamishe afungue ukurasa wa 85 kuna makisio ya mwalimu, mwalimu mmoja anatakiwa asomeshe wanafunzi 33 kwa mwaka 2017/2018. Lakini Mhe. Naibu Spika, hii mimi naiona hainipi picha nzuri, humu madarasani ukienda utakuta mwalimu mmoja ana darasa moja lenye wanafunzi 90 au zaidi ya 100. Sasa ukinijia hapa ukaniambia kwamba mwalimu mmoja anatakiwa asomeshe wanafunzi 33, bado mimi hapa nataka ufafanuzi zaidi. Ni kweli kabisa hii imepangika, lakini hawa walimu wako wapi, wamefichwa wapi, wako mijini, wamepewa wizara nyengine au wako wapi. Kwa sababu

ikiwa ni kweli kwamba mwalimu mmoja anatakiwa asomeshe wanafunzi 33 na ndio ilivyo hapa, basi haina haja tena ya kuajiri walimu. Sasa unakwenda kukuta mwalimu mmoja kapewa darasa lake zima, au madarasa yamechanganywa walimu wawili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika elimu ya watu wazima. Nimuombe Mhe. Waziri anieleze kwamba hayo madarasa yaliyojengwa ya watu wazima yamejengwa katika eneo gani, mbona sisi katika majimbo yetu wengine hatuna hayo madarasa hatuyaoni. Hayo madarasa ya elimu ya watu wazima hayaonekani. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri akija hapa atufafanulie aseme kwamba wewe Jimbo lako la Chonga kuna wanafunzi hapa na hapa kwa sababu mimi nawatafuta siwaoni hao wanafunzi watu wazima. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika elimu ya sekondari. Mhe. Naibu Spika, hapa tunatafuta walimu wa sayansi wa sekondari kama walivyosema wenzangu jana kwamba tutawatafuta walimu wa sekondari maisha. Kwa sababu elimu ya sekondari bado hakuna vifaa vya kusomeshea na walimu wa sayansi hawatapatikana. Mimi nimeona huku kuna skuli 14 tu ndizo zilizoingizwa vifaa vya kusomeshea sayansi, lakini ni zaidi ya skuli elfu moja vifaa hakuna wanafunzi hao wa sayansi watapatikana wapi. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri kama kweli unataka elimu ya sayansi ipatikane, basi tuongeze juhudi katika kuzipatia skuli vifaa

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika moja.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante. Baada ya hapo mimi nimuombe Mhe. Waziri atuelezee ile nyumba ya Madungu iliyojengwa ambapo pale ni kiwanja cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ile nyumba imejengwa na mtu binafsi, halafu inakodishwa wanafunzi pale, yaani wanakodi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kuwapa wanafunzi dakhalia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija hapa atuelezee ile nyumba ni sababu gani yule mtu akapewa pale kiwanja wakati kiwanja kile ni cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shaib Said Ali, anayefuata ni Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, ajitayarishe Mhe. Bahati Khamis Kombo na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa).

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo kuweza kuichangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, najua ni muda mchache. Kwanza nianze kuipongeza wizara ikiongozwa na mwanamke shupavu, jasiri na ambaye anatokea katika kada hii hii ya ualimu na elimu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo kwa wizara kupitia waziri wao, naomba niende moja kwa moja kwenye michango yangu. Mhe. Naibu Spika, naanza kwenye ukurasa wa 67 katika ubora wa elimu. Katika huu ubora wa elimu baadhi ya wajumbe wengi wameshauchangia, lakini mimi niombe sana tuboreshe miundombinu kwa watu wenye ulemavu. Katika kesi za watu wenye ulemavu tunaona kwamba kuna matatizo na changamoto nyingi zinazowakumba wenzetu

wenye tatizo hili la ulemavu, hasa ukiangalia watu wenye ulemavu wana mahitaji maalum, kwa hivyo watengenezewe miundombinu maalum ili na wao waweze kupata huduma hii kwa amani.

Mhe. Naibu Spika, watu hawa au wenzetu hawa wana upungufu na uhaba wa visaidizi, lakini sio visaidizi tu na hata wataalam, kuna walimu wanaojitolea kusomesha wanafunzi hawa na wanaojitolea kwenda kusoma, lakini wakirudi maskulini hawafanyi kazi ile ambayo wamekwenda kusomea. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niiombe sana wizara kupitia kitengo chake cha elimu mjumuisho, waweze kufanya mazungumzo baina ya walimu wanaokwenda kusomea kitengo hiki na wataalam wengine ili waweze kuwasaidia wenzetu.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana walisema walichapisha vitabu vya kusomea vya nukta nundu. Naomba niulize sana serikali je, vitabu hivyo vimegaiwa katika maskuli yepi. Kwa sababu tukiangalia kwenye changamoto kubwa ambazo tunazikuta maskulini, wenzetu hawa hawana vitabu wala *syllabus* za kuweza kuwasaidia. Kwa hivyo, atakapokuja hapa Mhe. Waziri tumuombe sana atuchanganulie na atuambie vitabu vile wamevigawa katika maskuli gani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna changamoto ya wanafunzi viziwi. Mhe. Waziri kwenye mipango yake anatuambia kwamba lengo la elimu mjumuisho ni kuwasaidia wenzetu ambao wana matatizo maalum, lakini kwa wanafunzi ambao wana ulemavu wa uziwi bado hatujaona msaada mkubwa na nguvu kubwa ambayo imewekwa kule. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tuna upungufu wa walimu wa lugha ya alama, walimu hawa naamini sana kuwa wanafunzi viziwi watawasaidia na watapiga hatua kutoka moja kwenda nyengine. Lakini kwenye hili naomba niwaulize wizara je, mnalijua hili kwamba kuna uhaba wa walimu wa lugha ya alama, lakini kama mnalijua mmechukua hatua gani ili kuona tunawasaidia wenzetu.

Mhe. Naibu Spika, sijamaliza dakika zangu naomba niende kwenye mikopo na elimu ya juu. Mhe. Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla jana alizungumzia kidogo kuhusiana na upandishwaji wa ada katika vyuo vyetu. Mhe. Naibu Spika, kuna matatizo kwa baadhi ya wanafunzi kukosa kuendelea na masomo yao kwa tatizo la kuongezewa ada kati kati ya masomo yao.

Mhe. Naibu Spika, hili nimeona nilizungumze kwa sababu miongoni mwa waathirika ni sisi vijana ambao tunaanza maisha yetu kwa ku-*engage* katika elimu. Natambua kwamba hizi ni sheria katika vyuo, ni vyema tukakaa na wanafunzi tukajaribu kushauriana nao na kuwaambia *situation* yoyote ambayo inatokea kuhusiana na mustakabali wa maisha yao na masomo yao. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niiombe wizara ikae na baadhi ya vyuo ili kuona utaratibu huu unakwenda vizuri bila ya kuathiri wanafunzi ambao wapo kati kati ya masomo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali. Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutuanzishia elimu mbadala, lakini kwa kutuanzishia vyuo vya amali ikiwa ni sababu au njia moja ya kuweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, tumeona na tumshuhudia katika ripoti yetu hii kuna changamoto ya kutokuendelea kwa majengo ya Daya, lakini kuna jengo la Makunduchi. Mhe. Waziri kupitia

wizara yako, mimi niseme kwamba majengo haya hayaendelei, na hayaendelei kwa sababu ikikaribia …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika moja.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Ikikaribia kipindi cha bajeti tunaanza kuona wataalam wetu wanaanza kujishughulisha, na mimi naamini hapa tukishamaliza bajeti majengo yale hayatoendelea. Kwa hivyo, niombe sana akija hapa Mhe. Waziri atuchanganulie ni lini Chuo cha Amali Daya na Chuo cha Amali Makunduchi vitaanza kufanya shughuli zake. Kwa sababu ninachoamini mimi sasa ni miaka saba, kwa hivyo tuangalie jitihada ambazo anazichukua Mhe. Rais, ili tumuunge mkono kwa kuweza kuwapatia fursa hii vijana wenzetu na hasa kwenye Mkoa wa Kusini na Daya kule Mtambwe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya vijana wenzangu wa Mkoa wa Kusini Unguja naomba niunge mkono hotuba hii baada ya Mhe. Waziri kuja hapa na mchanganuo mzuri kwa yale ambayo tunahisi tuna wasi wasi nayo kwa maslahi ya vijana na taifa kwa ujumla. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, atafuata tena Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) na ajitayarishe Mhe. Maryam Thani Juma. *(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wake wote wakiwemo Makatibu na Maafisa Wadhamini kwa utendaji wao mzuri ambao wametuonesha katika kitabu chao hiki.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika majengo yetu ambayo tuliyonayo katika wilaya zetu. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimshauri sana Mhe. Waziri kwamba hivi sasa tunajenga majengo ya ghorofa, lakini tunasema kwamba huko nyuma tayari tumeshajifunza, majengo yetu yaliyojengwa majengo matatu ambapo jengo moja Ngwachani skuli ya maendeleo, jengo la Dkt. Omar Ali Juma na jengo la Madungu. Majengo yale yalitupa changamoto sana na hasara kubwa ambayo tulikula kutokana na fedha ambazo wanatusaidia wenzetu wa nchi za nje. Mhe. Naibu Spika, naomba sana majengo haya ambayo tunajenga hivi sasa basi na nyinyi muwe karibu nayo sana ili kuona kwamba yale majengo yapo katika kiwango kizuri.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu Mhe. Naibu Waziri kwamba katika majengo ambayo hayana kiwango ni jengo moja la Skuli ya Dodo, lile jengo lilijengwa na mtu binafsi na yeye pia akaomba lile jengo liingie katika mkono wa serikali. Lakini hivi sasa lile jengo Mhe. Naibu Spika, lipo katika hali mbaya na linahitaji ukarabati wa hali ya juu sana. Namuomba Mhe. Waziri na Naibu Waziri waweze kufanya ziara ya makusudi ili kwenda kuliona jengo lile.

Mhe. Naibu Spika, nije moja kwa moja katika suala la walimu ambao wanakaa sehemu za mbali. Mhe. Naibu Spika, kuna walimu baadhi yao kwa kweli tunawapa mtihani mkubwa wale ambao wanakaa masafa ya mbali na wanavuka mito. Mfano mkubwa ni Skuli ya Mtangani, nilikwenda

kuitembelea skuli ile lakini nikakuta baadhi ya walimu hawakuweza kufika kutokana na masafa ya mbali ambayo wanakaa na wanavuka mito. Wapo walimu ambao wanakaa sehemu za Kiwani kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa kwao wakati wa mvua kubwa.

Mhe. Naibu Spika, niombe tu kwamba wapo walimu ambao wameshasoma na wapo katika shehia za karibu, basi nimuombe sana Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri waweze kuajiriwa wale, ili wale ambao wanakaa katika masafa ya mbali wapunguziwe masafa.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika elimu mbadala na elimu ya watu wazima. Mhe. Naibu Spika, nimeona humu ziko fedha nyingi ambazo zimetengwa kwa elimu mbadala na elimu ya watu wazima. Kwa hivyo, atakapokuja Mhe. Waziri aniambie katika Wilaya ya Mkoani ni sehemu gani ambayo wamefaidika na fedha hizi. Sikusudii kuzuia kifungu, lakini namuomba sana Mhe. Waziri atupe mchanganuo ambao utaweza kuwasaidia wale wenzetu wanaosoma kisomo hiki cha watu wazima.
Mhe. Naibu Spika, kwa kweli katika Jimbo langu la Chambani wapo wanakisomo cha watu wazima katika Shehia ya Wambaa eneo la Kutukuu, wale watu wana mfano mzuri na wanahitaji kupewa msaada mzuri, lakini sijawaona wananchi wale kusaidiwa. Kwa hivyo, nawaomba sana Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri waweze kufanya ziara waende wakatembelee madarasa haya ambayo wanasoma.

Mhe. Naibu Spika, nije moja kwa moja katika suala zima la kufeli kwa wanafunzi na kufaulu kwa wanafunzi. Nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba waliweza kufeli watoto wengi na waliweza vile vile kupasi watoto wengi sana tukawapigia mfano kwa mwaka huu wa 2016/2018. Lakini ulionesha mashirikiano mazuri wewe, Naibu Waziri wako, Makatibu wako pamoja na Maafisa Wadhamini wote waliomo katika wilaya zetu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba ndani ya skuli zetu wamo walimu na wamo wazee hawana mashirikiano na walimu. Kwa hivyo, nikuombe sana Mhe. Waziri uendelee na juhudi zako kama tunavyokusifu hapa, basi …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika moja.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, uweze kurudi tena chini kwa walimu na wazee kuwapitia na kuwaelimisha ili waweze kuwa na mashirikiano ya pamoja, ili jina lako lisiweze kupotea na liendelee kutajwa kama tunavyokutaja kwa sifa kubwa wewe pamoja na watu wako wote. Mhe. Naibu Spika, ahsante na nakushukuru sana, naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, nakushukuru sana Mhe. Bahati Khamis Kombo, sasa anayefuata ni Mhe. Maryam Thani Juma, baada ya hapo atachangia Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa).

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii kwa hotuba nzuri, pamoja na Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa maelezo mbali mbali yanayohusiana na elimu ambayo wametusomea.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuona ipo haja katika baadhi ya maskuli yetu kutujengea skuli za ghorofa. Mimi namshukuru sana katika jimbo langu nimebahatika kujengewa skuli hiyo na ujenzi unaendelea vizuri katika Skuli yangu ya Kizimbani.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika elimu ya maandalizi na msingi. Mhe. Naibu Spika, mara moja katika bajeti iliyopita niliwahi kulizungumzia suala hili na wenzangu tayari wamechangia, lakini na mimi naomba nigusie kidogo kuhusiana na elimu hii ya maandalizi ya watoto wetu kufanya mitihani darasa la sita.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wananchi wengi wanalilalamikia suala hili. Mhe. Naibu Spika, suala hili ni mtihani kwa watoto wetu. Ukiangalia watoto wetu ni wadogo wanaofeli wanabaki mitaani. Mhe. Shaib Said Ali amesema watoto wa darasa la kumi wamebaki, waliofeli wapo nyumbani. Naamini ni kweli kwa sababu sisi ndio tuliopo kwenye jamii na sisi Mhe. Waziri ndio tunaowaona wanafunzi wa darasa la kumi ambao wapo mitaani. Mara hii hapo mtaani kwetu tu wapo ambao wamefeli darasa la kumi na wamesema hawataki kurudia tena wameamua kubaki nyumbani, hili ni tatizo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia watoto wadogo wamebaki nyumbani wamesema hawawezi kurudia tena darasa la kumi. Sasa wizara itueleze kwamba kama wataendelea darasa la kumi na moja na kumi na mbili wanafunzi wale waliofeli darasa la kumi, hata kama watakwenda kule darasa la kumi na mbili, wanafunzi hawa kwa kweli hawawezi kuumudu mtihani wa darasa la kumi na mbili. Mhe. Waziri hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia wenzetu wa Tanzania Bara, ingawa masomo ya darasa la tisa na darasa la kumi tupo sawa, lakini huku msingi nadhani tupo tofauti. Sasa wanafunzi wetu tungewajenga huku chini kama wenzetu wa Tanzania Bara kwa sababu tunaona wenzetu wa kule wanafunzi wa darasa la saba wakija hapa utafikiria kwamba ni wa darasa la kumi na mbili. Lakini sisi hapa Zanzibar mtoto wa darasa la sita utasema kwamba ni darasa la pili kwa Bara, hili ni mtihani Mhe. Waziri. Mtoto wa Bara akija hapa wa darasa la saba ni sawa sawa na wa darasa la kumi na mbili, anakuwa kama mwalimu wa wanafunzi wetu sisi na sisi tunawaona. Hili ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaiomba wizara au serikali hili suala iliangalie kwa kina kwa sababu mfumo huu Afrika ya Mashariki tunaambiwa haupo, ni sisi tu Zanzibar tunauchukua mfumo huu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hili suala hebu awaelezee wananchi wetu kwa kina ili waweze kufahamu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika kitabu hiki cha bajeti kilichopita Mhe. Waziri alituelezea madarasa ambayo yataezekwa. Tumeangalia katika madarasa haya kitabu kilichopita ametwambia Skuli ya Sekondari Gando itaezekwa, lakini na bajeti hii tumeambiwa skuli hii pia itaezekwa. Naomba Mhe. Waziri anielezee itaezekwa mara ngapi kwa sababu naomba humu ipo na humu ipo, nataka wajue wananchi wangu wa Gando skuli hii itaezekwa mara ngapi au itaezekwa lini. Kwa sababu mara ile ametuelezea itaezekwa na mara hii ametuelezea itaezekwa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika skuli yangu ya Uvinje namuomba Mhe. Waziri kwanza skuli hii hali ni mbaya kuliko maelezo. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri maana sitaki niichambue mengi aende akaione hali halisi ilivyo. Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hichi cha bajeti ametwambia kwamba skuli hii imo katika ukusanyaji wa vifaa, mimi nataka nijue ukusanyaji huu wa vifaa ni kwamba wizara mnakusanya vifaa vya ujenzi au wananchi wanakusanya vifaa vya ujenzi wizara mkajenge au vipi. Mhe. Naibu Spika, nataka hapa Mhe. Waziri anielezee je, wizara ina mpango gani baada ya kukusanya hivyo vifaa vya kuijenga skuli ile. Kwa sababu skuli ile ina *foundation* ya vyumba sita, madarasa ambayo yanatumika ni vyumba vitatu tu sio vyengine na wanafunzi kila darasa moja madarasa mawili, kwa kweli ni mtihani kweli kweli. Leo mwalimu kikifika kipindi chake darasa moja litoke nje, aingie mwalimu asomeshe darasa jengine libaki lisomeshwe, baadae mwalimu wa kipindi chengine wa darasa jengine aingie ndani asomeshe, huu ni mtihani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, ni lini atakwenda kuitembelea skuli ile ili kujua changamoto walizonazo wanafunzi pamoja na walimu, pia madarasa haya sita mna mpango gani wa kuyajenga.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa walimu waliojitolea ambao ni wengi, hata mimi katika jimbo langu Skuli ya Mkote kuna walimu ambao wamejitolea.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika moja.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Walimu hawa waliingia tamaa wizara iliposema kwamba walimu wanaojitolea wapeleke vielelezo vyao ili kupata ajira, lakini hadi leo skuli hii haijapatiwa walimu hao waliojitolea na bado wapo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri waende wakafanye utafiti wa kina skuli ile, ili wajue walimu ambao wamejitolea na hadi hii leo hawajapatiwa ajira na tukiangalia ajira zinatoka.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia 80 na zilizobaki mpaka nipate majibu ya kina. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa), halafu ajitayarishe Mhe. Viwe Khamis Abdalla na baadae ajitayarishe Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii mbele ya ufalme wako. Kwanza kabisa mimi niende moja kwa moja kwa sababu sitakuwa na pongezi nyingi wote wamefanya majukumu yao ya kawaida, lakini nimsifu tu Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri sana aliowasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye vipaumbele ukurasa wa 4. Mhe. Naibu Spika, nimevutiwa sana na vipaumbele hivi vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na vimenifanya nisipige mabuti mengi leo kwa sababu furaha yangu ni kubwa sana. Lakini kimoja kati ya hicho ilikuwa kile kuwaajiri walimu wengi ambao wataajiriwa zaidi ya 470. Sasa hili limenivutia sana kwa sababu kipindi cha nyuma kama miezi miwili mitatu nyuma nilitembelea Skuli ya Kengeja. Skuli ya Kengeja msingi ina madarasa 28 lakini walimu 24, sasa kuna ukosefu wa madarasa mawili jioni na madarasa mawili asubuhi hayana walimu. Sasa hawa wakiajiriwa nadhani

watawaona kwa jicho la huruma ili tuone basi walimu wameelekezwa ili kuweza kunufaisha jamii.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hapa katika maandalizi na skuli ya msingi nataka niseme kuna kitu. Mustakbali wa vijana wengi kufeli maskuli, tunasema sekondari watoto wanafeli sana, lakini kwenye elimu ya msingi ndio kubovu kumechafuka. Kwa hivyo, niwaombe sana waangalie tulipoanguka wasiangalie tulipojikwaa, lakini tulipoanguka sasa ndio tuanze wapi, kwa nini tunafeli, kwa nini huku maandalizi tusiweze kuwaimarisha zaidi ili tukaona basi tumefanikiwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije kwenye elimu ya sekondari nitagusia gusia, nataka nizungumze kidogo tu kwenye sera lakini baadae niende kwenye bajeti. Elimu ya sekondari Waheshimiwa Wajumbe wengi wameshasema Skuli ya Kibuteni, lakini vile vile Madungu kamati yangu ilikwenda kukaa. Sasa hii ya Kibuteni mwaka juzi nilichangia na wakati nikichangia pale nilimwambia *AG* Mwanasheria msomi sana ndugu yangu kuwa avunje mkataba ule ili basi twende vizuri. Lakini mpaka mwaka huu ndio kwanza nyundo zimeanza kulia jana. Lakini hapa mimi nahisi kuna harufu ya rushwa sasa, katika wizara kwenye sehemu hii ya ku-*bid tender* kuna harufu ya rushwa inatokea.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa nia njema kabisa nitumie kifungu 111 kuweza kuomba Kamati Teule kwenda kuichunguza Skuli ya Madungu na hii ya Kibuteni. Ni muda mwingi kwa nini. Hata muda umekaa mwingi tunatupa sana jitihada za Mhe. Rais wetu kwa kushughulikia elimu. Hapa ningeomba sana.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 18 kwenye mafunzo ya amali na niwaambie tu kwenye sekondari na vyuo vikuu. Mheshimiwa niseme tu, kuna Chuo chetu cha Kiislam sasa hivi chuo kile tangu kuanza *process* mpya ya udahili ya *EVN* wale hawapati kuingia chuo chochote, walikuwa wanachukuliwa *degree* pengine ya Sheria kule *Zanzibar University*, lakini walikuwa wanaingia Al-Sumait kupata ualimu lakini sasa hivi hawapati. Mhe. Waziri atapokuja hebu aniambie kuna nini na vyuo hivi vyote kufungiwa na *NACTE* kuna nini. Hatui na elimu bora au kitu gani, maana hapa napo pana *conflict of interest* kati ya *NACTE* na *TCU* waweze kugombania mapato, hebu atwambie kuna nini asitufiche.

Mhe. Naibu Spika, niende tena kwenye elimu ya juu. Elimu ya juu niwapongeze sana *SUZA* lakini niipongeze pia serikali yangu kwa kuwa kuanzia mwaka 1999 tuna vyuo vikuu vitatu ambavyo vikubwa sana Zanzibar. Vile vile nimpongeze sana Prof. Idrissa Rai *VC* wa *State University* kwa kazi kubwa anayoichukua.

Mhe. Naibu Spika, nije tena kuna Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2009 Sheria Nam. 1. Mheshimiwa katika kipengele kimoja cha 50 kinamtaka Mhe. Waziri alete ripoti ya *SUZA* hapa Barazani ikiwa *financial report* au *dating report* pamoja na ripoti ya Makamu Mkuu wa Chuo. Mimi tangu nimeingia kwenye Baraza hili sijaiona, nikajaribu kukumbusha mwaka juzi angalau wenzetu waweze kutoa na Baraza lako tukufu likaweka maazimio Mhe. Naibu Spika, lakini pamoja na maazimio yale Mhe. Waziri amedharau Baraza lako na hapa naomba nikamate kifungu hiki cha *SUZA*, pamoja na mshahara wa Mhe. Waziri.

Nataka niukamate aniambie kuna nini ripoti haijaletwa mpaka sasa hivi. Na hii salamu sitoi kwake na hata kwa wengine wale ambao niliwataja kwenye hoja yangu kwa sababu wamedharau Baraza lako tukufu na mwaka jana tuliwaachia, lakini tumpongeze sana Mhe. Haroun Ali Suleiman, tumpongeze sana na Mhe. Salama Aboud Talib amejaribu kuleta ya *ZAWA*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka sasa nielekee kwenye viashiria namuomba Mhe. Waziri akamate buku kubwa katika kifungu KO33 katika ukurasa wa 3 kuna viashiria hapo, uwiano wa wanafunzi kwa walimu kazungumzia. Mwaka 2017/2018 amezungumzia mwalimu mmoja sawa sawa na wanafunzi 30, lakini mwaka 2018/2019 kaongeza tena 35, mwaka unaokuja wa 2019/2020 kaongeza 40. Sasa baada ya kurudi nyuma mimi nafikiri hiki kinanipa mashaka sana, takwimu hizi zinazoonesha hapa zinanipa mashaka, baada ya sisi kurudi nyuma na tukawa tuna uwiano mzuri sana sisi tumeanza kurudi *reverse* kuna nini. Viashiria vifanye nini. Mimi ningeomba tu Zanzibar hebu tuanzishe mjadala wa elimu, tunao kina Dkt. Bilal, Prof. Saleh Idrissa Mohamed na wengine wengi hebu tuanzishe mjadala wa elimu tuizungumze elimu yetu ikoje.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa huo huo kuna kiashiria cha kutoa mikopo kwa wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili zimebaki.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Nitajitahidi. Kutoa mikopo kwa wanafunzi. Hapa kutoa mikopo kwa wanafunzi imeandikwa kwa asilimia, asilimia ya mikopo iliyorejeshwa lakini hapa imeandikwa kwa pesa. Sasa sijui tunapimaje viashiria hivi tunakuwa hatuoni.

Mhe. Naibu Spika, nataka niende tena kwenye ukurasa wa KOK111. Hapa pesa ambazo zimeoneshwa mwaka jana makadirio haya ya mapato tumeoneshwa ni shilingi 143,093,000/= lakini safari hii zimeshuka imekuwa shilingi 104,000,000/= kwa nini zikashuka, hebu Mhe. Waziri atakapokuja atwambie.

Vile vile twende kwenye ukurasa wa KO114 anasema elimu ya maandalizi. Mwaka jana tulitengewa shilingi 70,724,571,000/=, lakini mwaka huu imeshuka sana tumewekewa shilingi bilioni 10 kuna nini. Naomba ufafanuzi huu.

Mhe. Naibu Spika, nina mengi sana kwenye KO115 kifungu PK0102 naomba ufafanuzi nitataja vifungu tu. PK0103 naomba ufafanuzi, lakini PK0104 naomba ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa KO116 naomba ufafanuzi katika kifungu cha HK01060202 Mfuko Maalum wa Kusaidia Huduma za Elimu. Mwaka jana umewekewa shilingi 2,500,000,000/= lakini safari hii umewekewa shilingi 400,000,000/= kwa nini zimeshuka hivyo nataka kujua.

Jengine nataka kujua katika kifungu ukurasa huo huo HK01060301 Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Elimu Pemba. Mwaka jana tuliwekewa shilingi 4,046,861,000/= lakini safari hii kumeshuka mpaka shilingi 2,611,000,000/= kuna nini hata zimeshuka hivyo.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwengine kote nitapeleka kwa maandishi lakini leo nataka kuuchukua mshahara wa Mhe. Waziri na ninaonesha nia ya kuondoa shilingi kwenye bajeti hii mpaka nipate maelezo ya kina. Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Viwe Khamis Abdalla na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri wake, Afisa Mdhamini, pamoja na watendaji wake wote. Moja kwa moja nianze mchango wangu na Chuo cha Elimu ya Amali ambacho kinatarajiwa kujengwa Daya, Mtambwe.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe wengi wa Baraza lako hili wameshakichangia chuo hiki cha Elimu Amali ambacho kinatarajiwa kijengwe katika Jimbo la Mtambwe. Mheshimiwa vijana wa Mkoa wa Kaskazini Pemba waliposikia kama kunataka kujengwa chuo hiki walifurahi sana na wakaweza kuipongeza serikali yao, lakini kwa malalamiko makubwa sana sasa hivi huu ni mwaka wa saba chuo hiki hata ule msingi bado haujaanzishwa katika sehemu hii ambayo ilitarajiwa kujengwa chuo hiki. Kamati yetu sisi wenyewe ni mashahidi tumekwenda na tumeona hali halisi iliyopo katika eneo hili ambalo linatarajiwa kujengwa chuo hiki.

Mhe. Naibu Spika, niiombe wizara wakisimamie chuo hiki ili kiweze kujengwa kwa wakati. Kwa sababu muda mrefu umeshapita vijana wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wanahitaji chuo hiki. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, vijana ambao wapo huko wana malalamiko ya ajira, lakini kama chuo hiki kitajengwa watakwenda pale kujisomea na wanaweza wakajiajiri wenyewe ili kuondokana na lile tatizo kubwa la ajira.

Mhe. Naibu Spika, niiombe wizara waache kutafuta wakandarasi ambao hawaishi katika nchi hii ya Zanzibar wanaturejeshea maendeleo yetu. Kwa sababu mkandarasi kama haishi hapa anaturejeshea maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika programu ya elimu ya maandalizi na msingi. Wajumbe wengi wameshachangia katika eneo hili, lakini na mimi naomba nichangie kwa sababu mimi mwenyewe nimeyashuhudia malalamiko ambayo wanalalamika vijana. Tulibahatika kukutana na vijana katika mikoa yote ya Unguja na Pemba wanafunzi na walituelezea malalamiko yao. Tulikutana nao na tukazungumza nao wakatueleza kwamba changamoto kubwa ambayo inasababisha wanafunzi wengi kufeli hapa Zanzibar ni msingi wa wanafunzi kwa sababu wanafunzi wanatakiwa waandaliwe tokea maandalizi mpaka kufikia elimu ya sekondari.

Mhe. Naibu Spika, vijana hao walisema tatizo kubwa au changamoto ni kukosa lugha ya Kiingereza katika masomo yao. Kwa sababu ili wanafunzi waweze kupasi vizuri katika mitihani yao ni lazima wajue kusoma somo la Kiingereza. Hili katika skuli zetu za Zanzibar halipo kabisa, mwanafunzi anakuja kusomeshwa darasa la nne au darasa la tano. Mhe. Naibu Spika,

naomba suala hili wizara waliangalie. Mhe. Naibu Spika, kama tunataka kweli Zanzibar tu-*improve* kwenye elimu basi somo la kiingereza lipewe kipaumbele katika kuwaendeleza viijana wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika majengo ambayo yanajengwa katika wizara hii ya elimu. Mheshimiwa niipongeze serikali kwa kujenga majengo ya kisasa kwa madhumuni ya kutaka kuondosha wimbi kubwa lililopo katika skuli zetu. Sasa hivi kuna Skuli ya Madungu kule Pemba ambayo tumeishuhudia kwa macho yetu inavuja kama pakacha, Skuli ya Chasasa ambayo ipo Wete pia hizi ni skuli za kisasa nayo hii inavuja. Mhe. Naibu Spika, Wizara iwaangalie wakandarasi ambao wanawatumia katika kujenga skuli hizi. Pia wizara iangalie wakandarasi wetu wa ndani wawatumie na wakandarasi tunao.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa kusema kuwa pamoja na matatizo yote hayo sisi kama kamati tulikutana na walimu na wakatupa malalamiko yao kuwa wazee pia hawana mashirikiano na walimu. Kwa hivyo, niwaombe wazee na wao kama wanataka vijana wao waweze kupasi vizuri basi wawe na mashirikiano na walimu ili kuweza kuimarisha elimu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, walimu pia walitulalamikia kuhusu Bima ya Afya kwa hivyo hili wizara pia walishughulikie. Mwisho kabisa naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Viwe nakushukuru sana.Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea tumepata wageni leo hapa Baraza la Wawakilishi na nimeona niwatangaze. Sasa wageni wenyewe ni wageni wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Wageni hawa ni Marais wa Serikali za Wanafunzi wa Vyuo mbali mbali vya hapa Zanzibar. Nao ni kama ifuatavyo:-

1. Ndg. Khamis Juma Khamis - Chuo Kikuu cha Al-Sumait asimame
2. Ndg. Abdulrahman Khamis Mussa - Chuo ni ZJMMC
3. Ndg. Salim Khamis Masoud - Chuo ni KIST
4. Ndg. Badru Suleiman Badru - Chuo ni MNMA
5. Ndg. Abdulhalim Mussa Jape - Chuo ni Microtech

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali tunakushukuru kwa kutuletea wageni hawa lakini naona kama vile usawa wa kijinsia haujazingatiwa. *(Makofi)*

Tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Masoud Abrahman Masoud, baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Said Omar Said na atafuata Mhe. Zaina Abdalla Salum.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Naibu wake, Katibu Mkuu, Manaibu wote wawili, Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, pamoja na Walimu Wakuu. Nimewashukuru kwa sababu namimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya

Ustawi wa Jamii tumefanya nao kazi karibu miaka miwili na nusu wametupa ushirikiano mkubwa viongozi wote niliowataja hapa.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Programu ya Elimu Mbadala. Mheshimiwa kama walivyotangulia kusema wenzangu kwanza niwapongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na hasa kwa kuangalia suala zima la elimu mbadala. Mwaka wa mwanzo tulipoanza kupita kwenye kamati yetu tulikuta hali haipo vizuri, lakini sasa hivi vituo vyote tulivyopita vya elimu mbadala mabadiliko yameonekana na mabadiliko ya ufanisi mkubwa.

Mhe. Nsibu Spika, tulipopita Mkokotoni palikuwa na wanafunzi karibu kumi naa mwaka wa mwanzo lakini sasa hivi kuna wanafunzi karibu mia tano, mia sita ambao wapo katika chuo kile. Wakati ule kulikuwa na hali kidogo ilikuwa finyu ya bajeti vijana wale walikuwa hawapati ile milo mitatu ambayo anatakiwa ale binaadam, lakini kwa sasa mafanikio makubwa yamepatikana na wanakula vizuri na wao wanasoma vizuri. Kwa hivyo, tuwapongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Jitihada zaidi zinatakikana kwenye suala zima la vitendea kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mzunguko wetu hapo tulifika mpaka Forodhani tuliwakuta vijana wanafanyakazi nzuri za kudarizi na kuchonga pale wakatupa maelezo mengi na sisi kama kamati tukajiridhisha. Yale maagizo tuliyoagiza sisi kama kamati wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wameyatekeleza. Palikuwa na mashine ya muda mrefu pale inatakiwa itengenezwe kwa ajili ya kupasulia mbao tumshukuru Mwenyezi Mungu mara ya mwisho tulipopita tayari imeshafanikiwa, kwa hivyo niendelee kuwapongeza na waendelee kuwasaidia vijana wale ili waweze kumaliza masomo yao na watakaporudi mitaani waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ipo kidogo kwenye suala zima la upatikanaji wa vyarahani, vyarahani tuliambiwa vipo tukapita kwenye stoo zao vyarahani vingi ni vibovu na waliahidi kuvitengeneza. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri asimamie hili ili vijana wetu wale wanaojifundisha kushona isiwe charahani moja inasubiriwa na vijana kumi. Waweze kupata vyarahani ambavyo watakuwa wanajifunza kila mmoja anapata muda mzuri wa kujifunza.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nizungumzie suala ambalo wenzangu wengi na huu umekuwa kama wimbo wa taifa suala la majengo yetu. Majengo yetu sasa hivi kila tunapoondoka kamati kwenda kuangalia kwenye hizo shule ambazo zinalalamikiwa kwa kweli hali sio nzuri. Fedha ambazo zinajengewa pale serikali nyingine tunatoa sisi wenyewe kama kodi lakini nyingine tunapewa na wahisani, lakini zile bado ni fedha za wavuja jasho tunahitaji tuzitunze vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika hili niiombe serikali iandae utaratibu iundwe timu hasa au kamati maalum iwe inafuatilia suala la majengo, majengo tunakabidhiwa muda wa miaka miwili lakini ukienda jengo linavuja kwa kweli jambo hili linatupa changamoto kubwa sana. Kwa hivyo, niiombe srikali iunde kamati maalum ambayo itafuatilia suala zima la majengo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka niseme ni suala zima la ukosefu wa walimu wa sayansi. Mheshimiwa wenzangu wamelizungumza lakini sisi kama Wajumbe wa Kamati kila

tunapopita na mara hii tuliamua kupita wilaya zote, kila wilaya unayopita kilio ni walimu wa sayansi. Niiombe serikali pamoja na kuwa inajitahidi kusomesha hao vijana lakini pia tunapata na wafadhili wanatusaidia kutuletea walimu, lakini bado serikali iweke mkakati mzuri sana kuhakikisha tunawapata walimu wa sayansi.

Mhe. Naibu Spika, pia suala jengine la uhamishaji wa walimu kiholela. Baadhi ya skuli kunakuwa na walimu wanakuwa tayari wameshazoweana na Wajumbe wa Kamati ya Skuli lakini pia wameshazoweana na wanafunzi ambao wanwasomesha. Lakini inapokaribia mitihani mwalimu yule anapokea barua ya uhamisho kutoka skuli ile kwenda skuli nyingine. Kuhamishwa ni kwa mujibu wa sheria mwalimu unaweza kumhamisha lakini tuangalie na uzito wa mwalimu unayemhamisha na uangalie uzoefu uliopo pale. Kwa mfano, kuna Skuli ya Mwenye - Kitundu kwenye Wilaya ya Magharibi "A" kwa miaka sita mpaka kumi iliyopita huko nyuma ilikuwa inapasisha wanafunzi wengi wa msingi pamoja na sekondari, lakini kwa bahati mbaya sana mwaka huu katika skuli za mwisho kwa Tanzania ni skuli hiyo ya Mwenge. Skuli hiyo kuna walimu sisi wenyewe tunawahitaji waje pale watusaidie. Kwa hivyo, niombe suala hili la uhamisho wa mara kwa mara Mhe. Waziri pamoja na afisa ambaye anahusika na suala zima la uhamisho wa walimu wajitahidi wale walimu ambao tunahisi tunawahitaji kwa wakati ule wabakie pale ili wasaidie vijana wetu wasiwahamishe haraka.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la upatikanaji wa vyoo kwa kweli kamati kila tunapopita kwenye skuli kwenda kukagua suala la vyoo ni tatizo, kuna baadhi ya skuli nyingine wanafunzi wa kike peke yao kwenye skuli ambayo ina wanafunzi karibu 1,600 wana matundu mawili tu ya vyoo, wanafunzi wanaume wanaambiwa wakajisaidie mwituni. Kwa kweli hali si nzuri tunaongeza mabanda lakini na vyoo tuviangalie sana.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la vitabu vya kusomea baadhi ya skuli kwa kweli wana masikitiko vitabu ni kidogo tuiombe wizara wajitahidi suala zima la vitabu vipatikane ili vijana wetu waweze kujisomea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nilitaka niliguse haraka haraka niipongeze Wizara ya Elimu kwa kufikiria suala zima la kuwasimamia suala la walimu wa madrasa, kwa kweli suala hili ni zuri sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nikupongeze kwa kuchunga sana wakati, lakini pia niseme kuwa na mimi naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Said Omar Said na baada ya hapo tutampa nafasi Mhe. Zaina Abdalla Salum, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ambaye ametujaalia sote uhai na uzima. Lakini pia nimpongeze sana

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kutokana na kwanza uwasilishaji wake. Lakini niwapongeze sana watenadji wote wa wizara hii kutokana na kazi yao tunayoiona humu wanayoifanya kwa kila siku.

Mhe, Naibu Spika, mimi nataka moja kwa moja niende kwenye Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali. Hapa nataka nichukue nafasi ya kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutujengea Kituo cha Elimu Mbadala eneo la Wingwi. Wingi ni *centre* kwa Wilaya ya Micheweni kwa hivyo kitu kipo pahala hasa sio pa majaribio. Kituo cha Walimu *(TC)* kipo Micheweni ambacho kimewakomboa walimu wengi wa Wilaya ya Micheweni. Lakini na Chuo cha Ufundi kipo Wilaya ya Micheweni ambacho kimewakomboa vijana wengi wa Pemba katika kila kona. Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ipo Wingwi ambayo imesambaza miradi mingi ya maendeleo katika kila kona ya Wilaya ya Micheweni. Lakini pamoja na hili jengo lililojengwa juzi la Elimu Mbadala pia lipo Wingwi, ndio nikasema pale ni pahala pake hasa jengo lile limepatikana pale.

Mhe. Naibu Spika, si kwa sababu ya kuwa ni *centre* tu lakini pia *population.* Wingwi ndio eneo pekee kwa Pemba ambalo lina idadi ya skuli saba ambazo zote wanafunzi wanajaa. Lakini si hilo tu pia Wingwi kuna muamko wa kielimu. Kama yupo Mhe. Haroun Ali Suleiman anaijua historia ya Wingi vizuri, wakati yeye ni Waziri wa Elimu. Wingwi imechukua nafasi ya kwanza kwa muda wa miaka mitano mpaka ikawahamasisha vijana wote Pemba kuja kuchukua masomo yao Wingwi na mpaka hivi ninavyosema hiki chuo bado wapo watu mpaka wa kutoka Mkoa wa Kusini. Hichi ni chuo kitakachowasaidia vijana wote wa Pemba kwamba wote wanapenda kusoma Wingwi kwa sababu wanajua wanaposoma Wingwi, watu wa Wingi ni watu wakarimu. watu wa Wingwi ni wenye kupokea wageni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo naiomba Serikali Kuu ituondoshee changamoto zilizokabili kituo hiki, yaani kukosekana kwa walimu wenye fani zinazohusiana na hicho chuo. Kwa mfano fani ya ujenzi, umeme, fundi bomba, ushoni na upishi. Kutokana na wakati huu tulionao vijana wengi sasa hivi mambo matatu ndio sana wanayoyapigania, kwanza ujenzi kwa sababu huu ni wakati wa kujenga. Kila mmoja anahitaji ujenzi, kwa hivyo tunahitaji angalau kama wizara bado haijajiweza basi tusikose walimu angalau watatu wenye fani tatu, yaani mwenye fani ya ujenzi, wenye fani ya umeme na mwenye fani ya fundi bomba. Haya ndio aghalabu sana yanayopapiwa na vijana wetu. Naamini kwamba mambo yakitengenea pale, basi chuo kile kitachukua au kitakuwa kinahudumia vijana wa Pemba nzima nina hakika asilimia 95.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika moja.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante. Nikitoka hapo nije skuli yangu ya Sinzini. Mheshimiwa kikao kilichopita nilimuomba Mhe. Waziri aitupie macho ile Skuli ya Sinzini ambayo banda lile lililojengwa kwa muda wa miaka mingi nyuma. Napenda nimueleze Mhe. Waziri kwamba nusu moja mimi nimeshaiezeka, sasa namuomba sehemu iliyobakia ya kuezeka nusu ya pili na kumalizia anisaidie mzigo huo. Namuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wingwi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Zaina Abdalla Salum na nimesema mchangiaji wa mwisho atakuwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii adhimu kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uzima na afya njema kwa kuweza kufika hapa na tukaweza kuchangia mambo yetu kwa ufasaha zaidi na kuweza kupitisha bajeti zetu za wizara mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie katika michango yangu kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuhakikisha kwamba anaweza kutelekeza majukumu yake kwa ufasaha zaidi hasa kuhusiana na sekta ya elimu, kuhakikisha kuwa sekta hii inawafikia walengwa na katika maeneo mbali mbali. Kwa kweli ameweza kuitimiza na sisi wenyewe ni mashahidi tumeona maskuli hivi sasa yanapatikana kila mitaa au kila sehemu vijijini na mijini, imeweza kupunguza changamoto za mrundikano wa wanafunzi katika madarasa.

Lakini Mhe. Spika, mimi kwanza nina kilio changu kikubwa kwa watu wenye ulemavu nachangia katika programu hii ya tano ambayo inazungumzia uboreshaji wa elimu katika programu ndogo ya elimu mjumuisho. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni moja ya nchi ambayo iliyoridhia mikataba ya Umoja wa Kitaifa kuhusiana na kuwasaidia au kutimiza sheria au kutimiza haki zote za msingi katika watu maalum yaani watu wenye ulemavu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, sekta ya elimu kwa watu wenye ulemavu wamekuwa hawaipati kwa ufasaha hasa kuhusiana na elimu ya mjumuisho. Katika utekelezaji wake Mhe. Waziri amezungumzia kwamba ameweza kutekeleza majukumu na kununua mashine ambazo za kuweza kuandika maandishi ya nukta nundu pamoja na kompyuta, lakini hakuelezea humu mashine hizo ni ngapi na kompyuta hizo ni ngapi na zimegaiwa sehemu gani, skuli gani na skuli gani zilizopata.

Pia katika utekelezaji wake wa bajeti iliyopita amezungumzia kuhusiana na kuwapa mafunzo walimu wanane ambao wanne Pemba na wanne Unguja, lakini walimu hawa hawakujulikana wamepelekwa katika maskuli gani. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, walimu hao wanapopata mafunzo wanakuwa hawatekelezi majukumu yao ipasavyo hasa ukizingatia watu wenye ulemavu wana matatizo kwa mfano wenye matatizo ya akili au uziwi. Walimu hao wanapokwenda kusomea lugha za alama wanakuwa hawatekelezi majukumu yao hatimae wanaomba uhamisho wanahama katika maskuli yale.

Mhe. Naibu Spika, hili suala tumelizungumzia sana na tumeweza kuuliza maswali mengi na hatimae Mhe. Waziri akatoa ahadi kwamba atalifuatilia vizuri kuhakikisha kuwa watu hawa wanaweza kupatiwa elimu ya ufasaha katika skuli hizo, lakini bado changamoto ndio kwanza zinazidi. Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, Skuli ya Mwanakwerekwe ni skuli ambayo inajulikana ilikuwa ikisomesha watu wenye ulemavu viziwi tokea enzi hizo, lakini hivi sasa ndio imekuwa ina changamoto kubwa sana katika kuwanyanyasa viziwi hao.

Mhe. Naibu Spika, skuli hiyo ina walimu wawili lakini walimu hao hukaa maofisini wakawa hawasomeshi na hatima yake wanapoingia katika maskuli wanazungumzia tu kwa mdomo mtu mwenye ulemavu anakuwa hafahamu, wanapokuwa hawataki kuingia basi wale wanafunzi wenyewe wanatoka wanawasaidia walemavu kuwasomesha, hii kweli ni haki Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakizuia kifungu hichi kisipite kwa sababu tutakuwa tunatoa fedha ili ziweze kuwatimizia watu hawa na matokeo yake zinakuwa hazifiki, na wala zinakuwa haziwafikii walengwa. Kwa hivyo, kifungu hichi nakizuia kisiweze kupitishwa tukubaliane na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu hili la tisa, tukizuie kifungu hiki ili kisiweze kupitishwa mpaka pale watakapokuwa watendaji wanaweza kutekeleza majukumu yao kwa miaka ya bajeti ya miaka ijayo basi tutaweza kuipitisha. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tumeshatoa ahadi sana na imeshazungumzwa sana na matokeo yake inakuwa hayatimizwi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende katika mambo ya mikopo nimpongeze sana Mhe. Waziri ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nakupa dakika mbili umalizie.

Mhe. Zainab Abdalla Salum: Sasa niende katika mambo ya mikopo nimpongeze sana Mhe. Waziri ambaye ameweza kutusaidia kupata mikopo ya elimu ya juu, lakini pia elimu hizi bado zina matatizo kwa sababu elimu ya juu hawezi kuipata kama huku chini hajaweza kuboreshwa vizuri. Nimpongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na watu wenye ulemavu kwa vile nawawakilisha watu wenye ulemavu, naunga mkono kwa asilimia sabini kwa vile kifungu hichi tunakizuia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Zaina na hongera sana kwa uwasilishaji wako. Mchangiaji wetu wa mwisho Mhe. Hamza nakupa dakika tano tu hazizidi dakika tano, naomba sana uwe makini katika uwasilishaji wako. Mhe. Hamza karibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuja hapa nikiwa mzima mwenye afya njema, halafu nakushukuru na wewe tu. Mhe. Naibu Spika, nasema mimi kwamba bajeti hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali siiungi mkono yote.

Mhe. Naibu Spika, kwanza inaonesha sijui kama wizara inatusikiliza tunapochangia au vipi, siku zote tunalalamika wanafunzi wetu wanafeli hivi na hivi tatizo tunalizungumza hapa lakini serikali bado haijalifanyia kazi, tujiulize wanafunzi ili wapasi wanahitaji nini, wapate walimu waliokuwa wazuri wametulia akili yao. Leo Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko ya walimu malimbikizo ya walimu kila pembe, kuna walimu wamestaaafu tokea mwaka 2016 mpaka leo hawajalipwa viinua mgongo, wewe utegemee hawa wanapokaa na wenzao watawasikiliza hawa walimu watafanya kazi kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nilikuja hapa kipindi kile nilikusanya data walimu waliokuwa wanadai malimbikizo karibu bilioni tano Waziri wa Fedha na Mipango sijui yuko hapa hapa na mtafuteni aje ajibu hapa. Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Fedha aliahidi kwamba watatoa fedha

walimu hawa watalipwa kwa awamu mpaka leo bado kelele hizi zipo, mimi nitakuwa na sababu gani ya kuunga mkono hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, kama waheshimiwa sote wawakilishi wa wananchi na walimu ni watu ambao wametupigia kura hapa, ili wanafunzi wetu waweze kupasi na walimu waweze kutuliza akili zao leo hapa bajeti hii tuirudishe. Au Waziri wa Fedha aje atwambie anatoa fedha zote ili walimu wapewe malimbikizo yao, lakini sio wale wastaafu tu lakini hata walimu ambao wanabadilisha madaraja. Leo walimu wetu wanaongeza taaluma mtu anatoka diploma anakwenda kwenye *degree* wengine wanakwenda mpaka *masters* kubadilishiwa mshahara mtu anafika miaka minne mitano anahangaika, wanafunzi watapasi wapi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hoja hiyo kubwa tena nzito tena humu mna walimu na wewe nafikiri ni mwalimu, maana yake ualimu haumaliziki mpaka unaingia kaburini. Kwa hivyo, walimu hawa kama hatujawatetea hapa tutawatetea wapi. Leo ndio maana utakuta watu wengi wanaona bora watoto wao wakawasomeshe skuli za *private* kwa sababu wanafunzi wametulia, walimu wametulia wanasomesha wanalipa husikii manung'uniko ya kulalamika malimbikizo au vitu gani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa umeniambia dakika tano nakwenda katika eneo jengine siungi mkono tena kuhusu suala la ujenzi wa majengo ya skuli za sekondari mabovu. Mhe. Naibu Spika, hizi pesa ni kodi za wananchi leo wakandarasi, tena naunga mkono hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed naungana nae tunaunda hapa Kamati Teule. Haiwezekani leo kampuni imeshatujengea maskuli mabovu yanavuja halafu leo wale wale wanakwenda kupewa kazi nyengine kwa kigezo gani. Mimi ninavyojua Mhe. Naibu Spika, kuna mambo matatu katika ujenzi kuna *contractor* halafu kuna *consultancy* halafu kuna *client* ambaye ni serikali, kwa hivyo serikali haiwezi kulipa pesa bila ya kuridhika na kazi inayofanywa na *contractor*. Leo inakuwaje *consultancy* anaiandikia serikali anapeleka *certificate contractor* analipwa wakati majengo mabovu halafu leo mnampa tena kazi, hii pesa leo hapa hatuipitishi Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika maboresho ya skuli. Mheshimiwa bajeti hii sioni hata sababu ya kuipitisha kwa sababu katika maboresho yote ya skuli, Skuli ya Shaurimoyo sasa hivi imeshazeeka kama ingelikuwa mtu anaendea kwa gongo, ile skuli imeshachoka. Tumeshakwenda pale na Mkurugenzi wa Elimu Suleiman Njeketu sijui kama yupo au ameshastaafu, kama nae ameshastaafu ana malimbikizo yake ameshalipwa au vipi. Tumekwenda tukakagua mkanipa maneno mazuri. Mimi nilitegemea katika hizi skuli za ghorofa zinazojengwa nitaambiwa na ile skuli yangu ya Shaurimoyo itapigwa mchi tutajengewa Skuli ya Shaurimoyo, lakini hata kwenye kitabu haimo na Mhe. Waziri siku zote anapita pale pale anapokwenda kwake.

Mhe. Naibu Spika, katika hoja zangu hizo nisiwe pia mwizi wa fadhila nataka niwapongeze *SUZA* unajua isionekane kwamba Hamza anaichukia Wizara ya Elimu napenda lakini matendo inakuwa kidogo siyapendi. Nawapongeza sana *SUZA* wamefanya kazi nzuri sana na katika taasisi ambayo naipongeza sana Kamisheni yangu ya Ardhi. Tuna kazi ya kuangalia ramani ya Zanzibar lakini vile vile kuboresha miji ya Zanzibar. Kazi ile Mhe. Naibu Spika, watu walioifanya kwa vizuri sana ni Chuo Kikuu cha Zanzibar *(SUZA).* Mimi nampongeza sana Prof. Rai aendelee sana kijana yule Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu aweze kufanya kazi vizuri.

Leo vijana wetu wa *SUZA* sasa hivi katika Afrika ndio *pilot* inayochukuliwa kwa ajili ya kuendesha zile ndege zisizo na rubani *(drones)*.

Leo vijana wetu hawa tayari wameshakuwa ma-*expert* wameajiriwa mpaka Tanzania Bara na makampuni. Kama mmesikia kuna hospitali zilikuwa hazifikiki kwa ajili ya kupeleka madawa, wao ndio waliokodiwa kwa ajili ya kuendesha zile *drones* kubeba madawa kupeleka katika hospitali. Kwa kweli ni kazi kubwa ambayo wanaifanya nawapongeza. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa nini kila siku tunatafuta makampuni ya mbali wakati kuna makampuni ya wazalendo yanafanya vizuri. Mhe. Naibu Spika, lazima tuzungumze ukweli tatizo letu sisi Zanzibar tunajenga uchumi lakini uchumi ule pesa tunazitoa hazijulikani zinakokwenda.

Mimi nataka nimpongeze rafiki yangu swahibu wangu …

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya. Mhe. Shaame nakupongeza sana tunataka tuone *pilot* skuli yako unayoijenga kwa kujitolea kwa ajili ya Wazanzibari tutakuja kuiangalia *quality* yake na kama itakuwa nzuri mheshimiwa mimi kwa kweli unajua wala tusiseme labda upendeleo, bila ya shaka ataingia kwenye *tender* lakini tuangalie vigezo. Makampuni ambayo yameshafanya vibaya Zanzibar sasa hivi nafikiri nafasi yako ya kuyaondoa. Mhe. John Pombe Magufuli anawanyang'anya watu kazi kwa nini sisi tunaogopa hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli naunga mkono hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed tuunde Kamati teule twende tukaangalie majengo na tuajiri ma-*expert* twende nao. Lakini vile vile Mhe. Spika, katika suala zima la malimbikizo ya walimu pamoja na viinua mgongo hili mimi sitounga mkono bajeti hii mpaka Waziri wa Fedha na Mipango aje anihakikishie kwamba pesa ataziingiza kwa ajili ya kulipa madeni haya.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwapongeza viongozi wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naomba kuchangia kwa maandishi katika maeneo matatu ya hotuba yako kama ifuatavyo:

Jambo la mwanzo ni kuhusu umalizaji wa *Library* ya Skuli ya M/Makumbi. Kwa kupitia nguvu za viongozi wa Jimbo la Chumbuni tumeanzisha ujenzi wa *library* na umefikia hatua kubwa sana na bado sehemu ndogo sana ya upigaji wa plasta, sakafu chini na *ceiling*. Na kwa kuwa serikali kupitia Wizara huwa wanatoa fursa za kumaliza yale mambo mazuri ambayo tumeanzisha wananchi.

Tunaomba ahadi ya serikali katika kuyamaliza maana hadi juzi tuliambiwa tutamaliziwa *library* hiyo.

Jambo la pili ni kuhusu jengo la asili la Skuli ya M/Makumbi. Kwa kipindi kirefu sasa jengo hilo limekutwa halikaliki na kuwa gofu tu, kwa hali ya kawaida hatujaona utengwaji wa bajeti ya kulitengeza kwa mwaka huu wa fedha.

a) Je, kuna utaratibu gani wa kulijenga au kulifanyia ukarabati mkubwa jengo hilo kwa ajili ya matumizi ya kawaida kama hapo awali. Ukizingatia skuli ile ndiyo uliyosoma hata wewe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Jambo la tatu ni kuhusu hati kwa ajili ya majengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naiomba serikali ichukue hatua za makusudi za kuyatafutia hati za matumizi ya ardhi, kwa sababu yanaathiri sana na kusababisha migogoro mingi kwa skuli zetu, vyuo vyetu na kadhalika.

Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia sabiini tu mpaka pale nitakapopata majibu ya kuridhisha. Ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Pongezi kwako Mhe. Waziri, Naibu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Pongezi kwa Wizara kwa ujenzi wa Skuli yangu ya Maandalizi Magomeni wananchi wa Magomeni wanafarijika sana.

Mikakati ya ujenzi wa miradi ya ujenzi wa majengo ya skuli. Pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na wizara kwa juhudi.

Naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

- Wizara izingatie Sheria ya Manunuzi wakati wa kutayarisha mikataba ya ujenzi.
- Wizara kuwa makini wanapowateua Mainjinia wetu wa ndani kusimamia ujenzi, wengine wanatawaliwa na tamaa, wengine uwezo wao mdogo.
- Wizara iunde kamati ya kufuatilia utekelezaji wa mikataba kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi.

Vile vile, naomba nizungumzie kuhusu takwimu za uandikishaji wanafunzi wapya. Takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatofautiana na takwimu za Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Elimu: WK. 22,071
WU: 22,326
Jumla: 44,397.

Tawala: WK. 28,167
WU. 28,370
Jumla: 56,537.

Naomba takwimu za wafanyakazi wa elimu waliolikizo bila malipo.

Kuhusu suala la uajiri wa walimu wapya. Pongezi walimu wapya 282. Wizara ikae na walimu waliojitolea kuanzia miaka ya 2000 – 2016 iwasikilize. Hawa ni wazalendo ikiwezekana waandaliwe mazingira ya kuajiriwa.

Kuhusu suala la ufinyu wa nafasi kwa wafanyakazi kwa Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama vile:

- Baraza la Mitihani
- Taasisi ya Elimu
- Bodi ya Mikopo
- Ukaguzi.

Naomba kutoa ushauri. Wizara izingatie suala hilo kwa umakini mkubwa fedha za *OC* haziwezi kujenga ofisi za taasisi hizi.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mchango wangu wa maandishi kuhusu masomo ya watoto wa miaka minne (4) na miaka mitano (5) masomo yawe matano tu, Kiingereza, Kiswahili, Hesabu, Historia na Michezo masomo haya yanatosha.

Ukosefu wa walimu Skuli ya Ole walimu waliostafu ni 13, walioajiriwa wawili (2). Pia Mhe. Waziri hapana haja ya kuleta walimu kutoa Nigeria walimu wazalendo wa sayansi wapo Zanzibar tena wengi na hawajaajiriwa wapo mitaani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Waziri Skuli ya Micheweni ina mwalimu mmoja wa sayansi kuanzia *Form I* hadi *Form VI* na *Form I* ni madarasa zaidi ya 10 ukiacha II na VI. Nashauri walimu ambao mnaajiri wa sayansi Skuli ya Micheweni iangaliwe kwa jicho la huruma, ili tuwasaidie watoto wetu.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Waziri kuhusu suala la ghala la kuhifadhia vitabu Pemba. Suala hili ni changamoto kubwa sana inayopelekea hata wafanyakazi wale hawana hata pakukaa wanakaa katika miembe. Kipindi hichi cha mvua tunawaweka fungu gani.

Maghala Pemba yapo tele kwa mfano, Tibirinzi na kadhalika.

Mhe. Waziri, hapo naomba jibu thabiti zile ni pesa za serikali vitabu vinaharibika vimeparaganyika hadi kupelekea walimu wanapokwenda kuchukua vitabu kwa ajili ya skuli zao kushindwa na kuvikosa kabisa na kukata tamaa nakurudi bila ya mafanikio.

Mhe. Waziri naomba jibu kwenye suala hili.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Naunga mkono hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia asilimia mia moja, mambo haya yapewe kipaumbele.

Jambo la kwanza uwepo wa walimu *qualified*, vifaa vya kusomeshea, maslahi mazuri kwa walimu, *libraries* katika kila Wilaya pamoja na kupitia upya mitaala yetu ili iendane na wakati.

Vile vile, elimu mafunzo ya amali inahitaji kuongezewa mikakati kwani kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma mbali mbali ambazo ujuzi wake hupatikana kwa kupitia vyuo vya amali tunahitaji skills nyingi, ili vijana waweze kujiajiri wenyewe. Kila la kheri.

Mhe. Nassor Salim Ali: Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake bora uliojaa hekma na busara na kusimamia amani na utulivu katika nchi yetu na kuleta maendeleo makubwa katika sekta hii ya elimu Zanzibar pamoja na maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla.

Aidha, nimpongeze na kumshukuru sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kipenzi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kujenga Skuli ya Kisasa ya ghorofa iliopo katika Shehia ya Rahaleo, kwa kweli tunampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza vyema Ilani ya CCM kwa vitendo.

Pili nikupongeze wewe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kazi kubwa unaofanya katika kusimamia yema Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hakika unastahiki pongezi pamoja na Naibu Waziri wako Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri kazi mnayoifanya ni kubwa sana, hongereni sana, sana.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Waziri na Elimu na Mafunzo ya Amali, nampongeza pamoja na watendaji wake wote. Tatizo la walimu wanaojitolea ni muda mrefu. Kwa hivyo, tunakuomba sana wizara yako pamoja na serikali mulione kwa jicho la huruma kwa Skuli ya Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Vile vile, Mhe. Waziri pamoja na serikali kujenga skuli ya ghorofa Micheweni katika Jimbo la Micheweni, pia nikupongeze kwa kusimamia vizuri elimu ya watu wazima wanaoendelea vizuri na kuweza kupata elimu bora kwa wale waliokuwa hawajuwi kusoma wala kuandika.

Mhe. Waziri Chuo cha Kiislamu Micheweni tatizo la uzio bado halijamaliza linaleta usumbufu kwa wanafunzi kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Harusi Said Suleiman: Naomba nimpongeze hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nampongeza na Mhe. Waziri kwa kuiwasilisha kwetu kwa ufasaha.

Upungufu wa walimu ni mkubwa hasa katika skuli za msingi zilizoko vijijini na hao wachache waliopo hawana utulivu wa kufundisha, muda wa kufundisha wapo na shughuli binafsi zaidi. Nashauri waongezwe na maafisa wa elimu wanaohusika wafanye ziara za mara kwa mara kwa kuangalia ufanisi maskulini, kwani wanafunzi wanatoka madarasani na kuzurura.

Somo la Historia linasomeshwa lakini nashauri somo hili liwekewe walimu maalum, ikiwezekana wote walimu wa zamani ambao Historia kwa asilimia kubwa wanaifahamu kabla kuyasoma mengi yaliyomo katika vitabu vya historia wao wameyaona. Walimu hawa ndio wapewe somo la historia, kwani hawa walimu wadogo wasasa walioisoma historia, wengine

wanaichanganya na siasa na kupelekea kuwapotosha wanafunzi watoto wetu ambao ni tegemeo la taifa la baadae.

Tunashauri kitabu cha Historia kilichotayarishwa na Mhe. Ramadhan Omar Mapuri.

Namalizia, kuunga mkono hotuba kwa asilimia mia, ahsante.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nieleze Sera hii ya Elimu tulifuata nchi gani.

Tatizo la suala la matumizi mabaya ya fedha za mradi na Mshauri Elekezi ya walimu wa *ART* na wasayansi linatumika kinyume na utaratibu uliowekwa katika hotuba yako na kitabu kikubwa hakuna fungu la umaliziaji na wa mabanda mapya.

Je, kwa kuwa hakuna fungu hebu tueleze utayamaliza vipi.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Waziri upungufu wa walimu hasa walimu wa sayansi. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wale vijana wetu ambao wanatoka katika maeneo husika wenye masomo ya sayansi wapatiwe ajira.

Mhe. Waziri, kuna suala la uhamisho ambalo ni jambo la kawaida kwa kila mfanyakazi lakini cha kuzingatia muangalie uwiano na pia tumeweka Maafisa wa Elimu Wilaya tuwashirikishe tunapofanya uhamisho. Kwa kweli mwalimu atapangiwa kazi hafiki hata wiki anakuja na barua ya uhamisho hili ni tatizo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Afisa Elimu Wilaya Kaskazini “B” kapata ajali Kikao kilichopita niliambiwa atapewa vespa hadi leo ni lini atapewa. Walimu wanafanya kazi ngumu ambayo sisi wazazi inatuwia vigumu ipo haja maposho yao walipwe tena kwa wakati na wale wanaopatiwa nauli waongezewe.

Mhe. Waziri nakuomba uniambie kila mwaka vijana wangapi wanaomba nafasi za kujiunga na masomo ya msingi kila mwaka. Na wangapi wanakosa nafasi hizo. Kila siku idadi ya vijana inaongezeka si kwa wale waliofanyiwa sensa tu hata kwa watu ambao wanahamia.

Je, wizara ina mpango gani wa kufanya zoezi la makusudi kufanya sense ya kuwatambua vijana walioko mitaani wanaohitaji kujiunga na elimu ya msingi, ili kuandaa bajeti inayokwenda na hali halisi tuliyonayo.

i. Mhe. Wizara imesema imejenga maktaba 23 Unguja na 14 ni skuli gani zilizo bahatika kupata maktaba hizo.

ii. Kuwafundisha walimu 200 kumudu kufundisha madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi ni jambo zuri, lakini hatuoni tunawaongezea mzigo mkubwa walimu hao.

iii. Tumeanzisha skuli za maandalizi kila kwenye skuli ya msingi lakini hatukuzingatia walimu, inapelekea wanafunzi hao kukosa elimu kwani walimu hamna.

iv. Jaduweli Na. 4 limeonesha walimu waliosomea na ambao hawajasomea. Je, wizara ina utaratibu gani wa kuwasomesha hawa walimu ambao hawajasomea.

v. Ukurasa wa 85 jaduweli inaonesha idadi ya walimu, idadi ya wanafunzi na walimu kwa walimu Mhe. Waziri naomba ufafanuzi wa hii wanafunzi kwa walimu.

Naipongeze wizara kwa kupandisha kiwango cha ufaulu kidato cha 2 kutoka 59.4 mpaka 74.0 lakini Mhe. Waziri inaonesha matokeo ya kidato cha 4 wafulana 69.5 wasichana 65.8 bado watoto wetu wa kike tuwahimize wafikie sana na wanafunzi wa kiume. Kitu cha kufurahisha matokeo ya kidato cha 6 wavulana 87.5 wasichana 98.3 ipo haja tuwapongeze vijana wetu wa kike.

Vile vile, kuna skuli ambazo ukarabati uko katika hatua za maandalizi. Je, ni hatua gani imefikia ya maandalizi hayo.

Walimu kutofika skuli kwa wakati hili lipo na walimu wengine hawafiki kabisa kwani mwalimu mmoja huyo anafundisha zaidi ya skuli moja wakati ukiangalia kuna walimu wazuri wenye sifa hawapewi ajira.

Naomba kutoa ushauri wizara husika iwaruhusu walimu kujitolea na pale inapotokea ajira wapewe kipaumbele cha kupatiwa ajira.

Naunga mkono hotuba hii. Ahsante.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Nampongeza Mhe. Waziri kwa jitihada na utendaji wake tangu kuteuliwa mpaka sasa na *inshallah* Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na imani ya kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokana na utaratibu uliopo sasa wa watoto kutoka darasa la sita (*std 6)* mpaka kidato cha I *(form one)*. Naomba kutoa ushauri sana tuliangalie hili kwa jicho la tatu kwani badala ya kuipandisha imekua tumezidi kuishusha elimu kwa watoto kutokufahamu, lakini pia wanamaliza skuli wakiwa na umri mdogo sana kitu ambacho kwa wenye familia za kinyonge tunawasababishia matatizo hasa kwa watoto wa kike wanapokaa nyumbani na kukosa elimu huku umri bado ukiwaruhusu kuwa skuli, hivyo itapendeza zaidi wakipita kama zamani kwa std 7 na *Orientation Class*, ili kuzidi kuelewa.

Vile vile, nashauri kupunguziwa kwa idadi kubwa ya wanafunzi darasani (skuli za msingi) kwani wamekua wakikaa kwa idadi kubwa madarasani inayoipindukia mia moja, hii hata kiafya inahatarisha kwa watoto hao.

Nakutakia kila la heri katika kufanikisha upitishwaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa namna ya uongozi wake, jinsi anavyoiendesha nchi yetu, na kuweza kuwa na amani na utulivu.

Pili nampongeza Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri katika uongozi wao kwa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Tatu nampongeza Katibu Mkuu pamoja na Manaibu wake wote wawili akiwemo Afisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba. Naomba kutoa mchango mfupi sana, hususan kwa baadhi ya walimu kujifanya ni wanasiasa na kuacha kazi yao ya ualimu na kuhubiri siasa katika maskuli, hususan katika Mkoa wa Kaskazini kuna baadhi ya walimu wanatabia hiyo. Tunawaomba waache tabia hiyo, kwani wao wameajiriwa kusomesha sio kufanya kazi ya siasa. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hili iliangalie suala hili na kulifanyia kazi.

Baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mhe. Naibu Waziri wake na maafisa wa elimu.

Pamoja na kupongeza elimu sana katika jimbo langu na mimi katika bajeti ijayo skuli yangu ya Kangani, ili na mimi nipate skuli ya ghorofa kwa sababu skuli ya ghorofa ni jumla ya maendeleo.

Naomba muendelee kuimarisha elimu yetu Zanzibari.

Mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma, sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, nakupa dakika kumi ili Mhe. Waziri na yeye apate muda kama nilivyosema mwanzo leo Ijumaa naomba sana ujitahidi katika kuwasilisha majumuisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, maeneo mengi sana yamechangiwa na mimi katika muda huu nachukua fursa hii kufafanua baadhi ya maeneo hayo. Lakini kabla ya kufafanua nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Wawakilishi wenzangu kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuibua changamoto ambazo sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunapaswa kufanya kazi.

Nawapongeza kwa makusudi kuwaeleza kwamba kwa kweli sasa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa walimu kama sisi kwa hivyo nashukuru kwa dhati. Nasema hivyo kwa sababu watu wengi ambao hawako katika sekta ya elimu huwa mambo ya elimu hawayaelewi, lakini wawakilishi wetu wanaelewa kwa hivyo ni walimu wenzetu hongereni sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kwenda katika baadhi ya hoja na nitaanza kuangalia shughuli za upungufu wa walimu. Kwa kweli hii ni changamoto ambayo wizara tunaielewa na tunaifanyia

kazi na tumefanya kazi kubwa katika kipindi hichi tumeajiri walimu wengi na mchakato haujasita unaendelea. Kwa hivyo, tunategemea kwamba tutaweza kupunguza hatuwezi kukamilisha kipindi kifupi, lakini tunaweza kupunguza tatizo hilo. Labda nitoe mfano mdogo Mkoa wa Kaskazini Unguja tumeweza kuajiri walimu 254 ambao wamepangiwa skuli mbali mbali za mkoa huo wa Kaskazini. Lakini pia zoezi tunaendelea kwa hivyo tunatarajia kwamba tunaweza kupunguza hatua kwa hatua.

Lakini changamoto ni kubwa zaidi tunapokwenda katika maskuli ni walimu wa sayansi yaani wanasema walimu wa fani, lakini nayo pia tunaweza kuifanyia kazi. Hivi sasa wizara na baadhi ya Wawakilishi watakuwa wamesikia kupitia kwenye redio kwamba tumejaribu kuwaita ili kuwaratibu sawa sawa hawa wanafunzi wetu ambao wamemaliza masomo ya sayansi na zoezi hilo linaendelea na lina mwitikio mzuri. Kwa hivyo, tunategemea kwamba baada ya kuwapata hao basi taratibu nyengine za kuomba kibali zitafanyika.

Kwa hivyo, niseme kwamba utaratibu huu tumeufanya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA)* ili kuweza kuwafahamu wanafunzi hao na baadae kuwaombea kibali kwa ajira. Kwa hivyo, tukifanikiwa zoezi hili kwa kiasi fulani tutakuwa tumepunguza uhaba wa walimu hasa wa sayansi ambao ndio tatizo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la walimu wa sayansi kutoka Nigeria wamekuwa wakizungumzwa kwa muelekeo tofauti. Niseme kwamba bado wizara itaendelea kushirikiana na walimu hawa kwa sababu bado tuna upungufu katika masomo ya Physics na Mathematics. Mwanzo tulikuwa tukichukua kwenye Chemistry na Biology lakini tatizo hilo limepungua sasa tumebakisha kwenye Physics na Mathematics. Nitoe takwimu kidogo kuweka rekodi sawa kwamba uhusiano wetu huu umeanza mwaka 2013 ambapo tulipata Wanigeria 15, mwaka 2015 tulipata 33, mwaka 2017 tulipata 8 na sasa hivi 2018 mpaka sasa 15 kwa jumla ni 71 ambao wanakuja kwa nyakati tofauti hawakutani hawa, wakati mwengine wanakuwepo nane wakati mwengine kumi na tano na kadhalika.

Kwa hivyo, mpaka pale ambapo tutakuwa tumejitosheleza katika masomo hayo mawili hapo tutasita kuagiza. Kwa hivyo, hiyo ni taarifa rasmi na si sahihi kusemwa kwamba mtaagiza walimu 300 Nigeria, hiyo sio sahihi hata kidogo hakuna makubaliano ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu walimu wanaojitolea na ajira. Nadhani wajumbe mtakumbuka kwamba sheria ya utumishi pamoja na kanuni zake hazijaeleza kwamba sifa ya kujitolea ndio sifa ya ajira. Kwa hivyo, muajiri yeyote anatakiwa atoe tangazo katika vyombo vinavyoaminika juu ya ajira yake halafu baadae ziende taratibu nyengine zinazohusika, lakini kipengele hichi hakimo. Kwa hivyo, aneyejitolea na asiyejitolea ana nafasi sawa katika kuajiriwa kwa mujibu wa kanuni inayosimamia Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, kwa bahati nzuri katika mwaka huu pia wanaojitolea walipata ajira hiyo, lakini si kwa sababu ya kujitolea, ni kwa sababu ya vigezo vyengine vinavyotumika katika ajira ikiwemo Skuli ya Chaani pia wamejitokeza waliojitolea.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine nitalisema kwa ufupi sana, wengine walikuwa wanajiuliza kama hivyo ni kweli viko vituo vya elimu ya watu wazima katika nchi hii. Kwa kweli tunavyo viko dhahiri na vinaonekana. Viongozi mbali mbali wa Wizara ya Elimu huwa tunapata fursa ya kuvitembelea vituo hivi. Nisisitize kwamba vituo hivi vina kazi kubwa sana vimeongeza mapana

ya kazi zake, ndani yake humu kuna suala la ujasiriamali na ushirika, wale ambao tayari wameshajua kusoma a, b na c wanahamasishwa kuunda vikundi vya ushirika na wanawezeshwa na wanasaidiwa.

Lakini vile vile kuna programu za kuwawezesha wanawake ndani ya masomo. Kwa hivyo, vikundi hivi vipo na vinafanya kazi kubwa sana, na uhalali wa kuwepo huu unatokana na ukweli kwamba bado tunao baadhi ya wananchi wetu hawajaweza kusoma na kuandika. Hii inatokana kwamba kuna idadi ya vijana wetu mbali mbali ambao kwa sababu mbali mbali waliacha skuli njiani kwa hiyo haja ya kusomesha jambo hili lipo na litaendelea kuwepo, ingawa sasa hivi tumekaribia asilimia 85 ya watu wetu ya kuweza kujua kusoma na kuandika.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo nataka kulilisitiza kuhusu Vyuo vya Quran na Madrasa. Niseme kwamba sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunahusika zaidi na masuala ya usimamizi wa mitaala katika vyuo vya quran na masuala mengine yanashughulikiwa katika Ofisi ya Mufti. Kwa hivyo, kwa upande wetu sisi tunatoa misaada kadri inavyowezekana, tunatoa mafunzo, tunatoa semina katika mambo yanayohusu usomeshaji, mbinu za usomeshaji, nidhamu na mambo kama hayo, masuala mengine yote yamebakia katika Ofisi ya Mufti.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la Sera ya Elimu hapa tumekuwa na kauli ambazo wakati mwengine zinapingana, tunasema vijana wetu wanachelewa kusoma wanasoma watu wazima wanakuwa na *PhD* watu wazima. Kuna kauli inayosema kwamba vijana wetu wanaanza skuli mapema kwa hivyo wanafikia umri hawajiwezi kufanya lolote ni kauli ambazo zinapingana. Sera yetu imesema watoto wetu wasome katika umri mapema ili ikifika umri fulani wawe tayari wameshahitimu masomo yao. Sasa sera hii ndio ambayo kidogo tunatofautiana humu ndani. Mhe. Naibu Spika, kama tunataka vijana wetu wasome elimu mapema kwa hivyo sera yetu iko sahihi. La tunataka wachelewe kusoma basi kwa kweli inabidi tutoe maoni, maoni yatakayokuja baadae yanaweza kuzingatiwa. Lakini kwa kweli hawa wenzetu ambao tunasema wanahitimu mapema ni kutokana na mfumo kama huu ambao na sisi tunaufanya. Hata hivyo, Wizara ya Elimu inaendelea na zoezi lake la kufanya mapitio sera hii na wakati ukifika taarifa zake tutazitoa hadharani ili ieleweke kitu gani kimepatikana.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo limezungumzwa sana na nitataja Mhe. Hamza Hassan Juma na wengine wamelitaja kuhusu malimbikizo ya walimu.Walimu walikuwa na malimbikizo ya aina tatu, kwanza malimbikizo ya likizo, malimbikizo tunaita ya posho ya muda mrefu, na malimbikizo ya marekebisho ya mshahara. Niseme hili la malimbikizo ya likizo kwa kweli tumeweza kulifanyia kazi nadhani limefikia asilimia 90 tumeweza kulikamilisha, kulikuwa na malimbikizo toka 2013 lakini tumeweza kuyalipa kidogo kidogo mpaka sasa kwa upande wa Pemba tumefikia mpaka 2017 tumeshawalipa likizo zao na Unguja pia inakaribia 2016 mwisho mwisho. Kwa hivyo, zoezi hili linakwenda vizuri na si muda mrefu tutalimaliza.

Kulikuwa na malimbikizo mengine ya muda mrefu ya mabadiliko ya mishahara ya walimu waliongezwa na hii napenda niiseme kwa takwimu ili watu waelewe vizuri zaidi. Wizara imelipa malimbikizo kwa mwezi wa Machi na Mei, 2018 mishahara kwa watumishi wenye uzoefu wa miaka 30 kwa Unguja shilingi milioni 574,369,140/= hizi zililipwa mwezi wa Mei. Lakini pia na kwa upande wa Pemba tumewalipa pia walimu malimbikizo yao shilingi milioni 375,690,920/=.

Kwa hivyo, kusema kwamba hakuna deni tena la walimu kuhusu walimu ambao wana uzoefu wa muda mrefu katika suala hili. Kilichobakia sasa hivi ni malimbikizo yale yanayotokana na kurekebisha mshahara, amerudi masomoni Julai, *prosess* zikikamilika za marekebisho ya mshahara pengine Septemba hii miezi mitatu mitatu na kadhalika. Na hii tayari imeshaelezwa na serikali kwamba katika mwaka huu wa fedha pia nazo zikalipwa malimbikizo haya. Kwa hivyo, huo ni ufafanuzi kuhusu suala hilo.

Suala jengine ambalo lina mjadala ni kuhusu ubora wa elimu. Mhe. Naibu Spika, ubora wa elimu una namna yake ya kupima, ina namna yake ya kutafsiri na ndio kila mmoja ana tafsiri yake. Lakini hata hivyo, ubora wa elimu haufikiwi, unaoufikiri ubora wa leo kesho si ubora tena, kesho kutwa si ubora tena, kesho kutwa si ubora tena, kwa hivyo wanasema ni *flying* haipitiwi. Lakini tunachosema kwamba kama tutapima ubora wa elimu katika ujumla wake, yaani baada ya wahitimu kumaliza masomo na kuanza kufanya kazi utapata jawabu vizuri kabisa kama ubora wetu wa elimu uko vipi. Nitoe mifano naona, hebu tuangalie wataalam wetu mbali mbali tukiwemo sisi wanasiasa ambao tumetokana na mfumo huu huu tuko vipi katika kufanya kazi zetu. Maoni yangu tunafanya kazi sawa sawa, huu unatokana na huo mfumo wa elimu ambao tunauendesha na tunausimamia sawa sawa.

Madaktari wetu pia na wao wanatokana na mfumo huo huo wa elimu, waandishi wetu wanatokana na mfumo huu wa elimu, walimu wetu wanatokana na mfumo huu huu wa elimu. Kwa hivyo, tunapotizama mfumo wa elimu ubora wake tuutizame katika matokeo ya baadae. Kwa hivyo, kwa maoni yetu ni kwamba idadi kubwa ya wataalam tulionao Zanzibar inatokana na mfumo huu wa elimu tulionao, na wataalam hao imesemwa sasa hivi hapa kwamba wana sifa zinazojulikana dunia nzima wamesema baadhi hapa wakitambua. Kwa hivyo, bado nisisitize kwamba elimu yetu iko katika njia sahihi isipokuwa kuna changamoto zilizopo tuendelee kushirikiana kuzitatua. Hiyo naona ndio maoni ya Wizara juu ya jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, nieleze kwamba kuna suala la uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi na hii inakwenda kwa viwango, kiwango cha maandalizi pengine idadi ya wanafunzi inakuwa ndogo zaidi mwalimu mmoja wanafunzi 20, sekondari inakwenda kwa mujibu wa viwango. Lakini hiyo ni kinadharia, inapokuja hali halisi ndio tunaona kama hali hiyo baadhi ya skuli wanafunzi wanafikia 100, baadhi ya skuli wanakuwa 30 na kadhalika.

Sasa changamoto hii sisi wizara tunaielewa na tunajitahidi kuifanyia kazi na hatua zinazofanyiwa kazi moja ni hiyo kuongeza madarasa, tukiongeza madarasa tutapata fursa ya kuwapunguza wanafunzi wetu katika madarasa ambayo wamekuwa wengi zaidi. Kwa hivyo, hatua hizi tunakwenda hatua kwa hatua na inakwenda kwa mpango madhubuti unaoratibiwa vizuri sana katika Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho tuzungumzie suala la uvujaji wa majengo ambayo yalijengwa kupitia mradi wa Benki ya Dunia. Suala hili tumelifafanua vya kutosha na mwisho ikabidi sasa wizara iunde Kamati ya Uchunguzi juu ya masuala haya kipi kilitokea. Kamati hiyo tumeambiwa imeshamaliza kazi karibu wakati wowote itawasilisha ripoti yake kwa Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kwa hivyo, tusubiri kamati inasemaje katika kuona matokeo ya uchunguzi wenyewe.

Kwa hivyo, sisi wizara si kwamba tumefurahia, haturidhiki na ndio maana tukaunda kamati yenye wajumbe kutoka nje kabisa ya taasisi yetu ili kuona kuna tatizo gani, maana yake sasa hivi kuna maoni tofauti, kuna wanaosema kuna harufu ya rushwa, kuna wanaosema kwamba utaalam mdogo, kuna wanaosema kwamba *supervision* kulikuwa hakuna ufuatiliaji, wapo wanaosema kwamba michoro yenyewe sio, kwa hivyo kuna maoni mbali mbali. Kwa hivyo, tusibiri kamati itatwambiaje halafu baadae tutaelezana na hatua zinazohusika zitachukuliwa.

Mwisho kabisa, nirejee tena kauli yangu ya kuwashukuru sana, kuwapongeza sana Wawakilishi kwa kufanya kazi nzuri iliyotukuka. Kwa maana hiyo, sisi Wizara tunaheshimu sana maoni yenu na tutaendelea kufanya kazi kwa karibu zaidi kwa sababu siku zote sisi tuko karibu na wananchi na wananchi ndio nyinyi viongozi mliopo hapa. Ahsanteni sana. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru, sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye aje kufanya majumuisho. Mhe. Waziri karibu. *(Makofi)*

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Muongozo wa Spika.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu muongozo Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, leo ni siku ya Ijumaa kama ulivyosema, na siku ya Ijumaa hasa katika huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan tunatakiwa saa 6:00 kamili tuwe tumeshafika misikitini. Sasa hivi tuna muda wa saa moja na Mhe. Waziri hatujajua hotuba yake atachukua muda gani. Tatizo tukishaingia kwenye vifungu hatuwezi tena kuakhirisha Baraza mpaka tumalize. Sasa muongozo wako Mhe. Naibu Spika, sijui kama hutoona busara kwa sababu mambo tuliyoyazungumza yanahitaji majibu ya umakini na majibu ya uhakika yakafanyiwe kazi. Sasa hofu yangu kusema kwamba tumalize haraka haraka leo kutokana na muda …

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nimeshakufahamu kaa kitako. Kwa sababu tunachukua muda wa hayo maelezo sasa unataka kueleza mengine, nimeshakufahamu unachokisema.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya nimekuelewa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimemuelewa sana Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali tayari tumeshazungumza anasema atahitaji kama nusu saa haitozidi zaidi ya dakika arubaini kwa ajili ya majumuisho yake. Sasa baada ya hapo tutakuwa tuna muda tutapitisha vifungu. Mimi naamini kwamba kweli leo Ijumaa na kila mtu anataka kwenda msikitini mapema. Ningeshauri tutaongeza kama robo saa nyengine ambayo saa 6.15 au nusu saa itatosha watu wataweza bado kwenda kukimbilia misikitini.

Waheshimiwa Wajumbe tumejipanga katika wizara hii tunamaliza leo na mimi naamini muda utatosha kabisa. Naomba sana twende hivi tunavyokwenda na kama kuongeza muda hautozidi dakika 20, mimi naamini kabisa hivyo haitozidi. Kwa sababu Mhe. Waziri … Mhe. Hamza Hassan Juma tuache tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Samahani sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma kaa kwanza, kaa halafu na mimi nikae, kaa mimi nimesimama. Mheshimiwa wewe mwenyeji sana wa kanuni hizi, kwa hiyo naomba tuzifuate kanuni. Nilichokisema kwamba tutaweza kuongeza muda hautozidi hautokuwa umekiuka ule muda wa kwenda kusali. Waheshimiwa na msikiti tunao jamaa tunaweza tukaisalia hapa leo. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Muongozo.

Mhe. Naibu Spika: Naam kuhusu muongozo.

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, unajua tuna tatizo moja la Baraza letu kubanwa sana na kanuni zetu. Kama tulivyosema Mhe. Naibu Spika, tukishaingia kwenye vifungu hapa hata tutafika saa nane lakini hatuwezi kuakhirisha Baraza hilo lazima tukubaliane. Sasa hoja yangu Mheshimiwa, sisi hoja tulizozizungumza tumezungumza hoja nyengine zinahitaji takwimu, zinahitaji maelezo yaani jawabu za uhakika kabisa. Naamini kwa muda huu mchache buti hapa zitakuwa zaidi ya kiwango na huu muda wa robo saa hautokuja kutosha. Bora Mheshimiwa tumpe nafasi Mhe. Waziri aende akatafute majibu ya uhakika ili siku tunayokuja kupitisha bajeti yake inapita bila ya tatizo. Mheshimiwa mtu kama mfano umewapa watu dakika tano, tano …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma nimekuelewa sawa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kuna mambo mengi watu hawakuyazungumza wamezungumza kwa kifupi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma nimeshakuelewa na huna haja ya kueleza masuala mengi, nimeshakuelewa na nakubaliana na wewe tumuache Mhe. Waziri afanye majumuisho yake mpaka saa 6:00. Nimekubaliana na wewe kwamba tumalize saa 6:00 ili Mhe. Waziri tukija Jumatatu tupitishe vifungu. Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa muongozo wako ambao umeutoa ndani ya Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba Waheshimiwa Wajumbe hawana nia ya kuzuia mafungu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ila kilichopo ni kwamba kila mmoja anaumwa na elimu na kwa sababu tunajua kwamba elimu ndio msingi mzima wa maendeleo ndani ya nchi yetu.

Kwa hiyo, tumewafahamu Waheshimiwa Wajumbe na Wizara yetu wa Elimu na Mafunzo ya Amali iko vizuri kwa hili na inasimamia vizuri sana.

Lakini vile vile ni matumaini yetu kwamba Waheshimiwa Wajumbe tutakuwa tunashirikiana kadri siku zinavyokwenda kila siku kama tunavyoshirikiana, tutazidi kushirikiana ili kuona kwamba elimu ndani ya nchi yetu inakwenda vizuri sana kwa maslahi mema ya nchi yetu na vijana wetu wa Kizanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema leo hii tukaweza kukutana tena katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru binafsi wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kufanya ...

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa, Mhe. Hamza Hassan Juma, Waheshimiwa mmetaka kusikiliza majibu naomba msikilize majibu badala ya kuzungumza. Tusikilize majibu ya Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nikushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kufanya majumuisho ya michangio na ushauri mbali mbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya mwaka 2018/19.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana wajumbe wote ambao kwa namna mmoja ama nyengine wamechangia bajeti yetu hii wakiwemo wale ambao wamechangia moja kwa moja kwa kuzungumza na wale ambao wamechangia kwa njia ya maandishi na wengine naamini kwamba hawakupata nafasi. Lakini naamini kwamba michango mingi wanayo, lakini vile vile michango yao tunaiona ndani ya majimbo yao husika.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuanza kuwatambua wale wote ambao wamechangia hotuba yetu hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, waliochangia moja kwa moja ni 28 kwanza kabisa ni:

1. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
2. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
3. Mhe. Simai Mohammed Said
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf
6. Mhe. Suleiman Sarahan Said
7. Mhe. Shehe Hamad Mattar
8. Mhe. Abdalla Ali Kombo
9. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
10. Mhe. Ali Khamis Bakar
11. Mhe. Hidaya Ali Makame
12. Mhe. Panya Ali Abdalla

13. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
14. Mhe. Suleiman Makame Ali
15. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
16. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
17. Mhe. Shaib Said Ali
18. Mhe. Mussa Foum Mussa
19. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
20. Mhe. Bahati Khamis Kombo
21. Mhe. Maryam Thani Juma
22. Mhe. Mohamed Said Mohamed
23. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
24. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
25. Mhe. Said Omar Said
26. Mhe. Zaina Abdalla Salum
27. Mhe. Hamza Hassan Juma
28. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri)

Vile vile Mhe. Naibu Spika, wapo waliochangia kwa njia ya maandishi wakiwemo hawa wafuatao:

1. Mhe. Ali Salum Haji
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo (Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale)
6. Mhe. Hamida Abdalla Issa
7. Mhe. Harous Said Suleiman (Naibu Waziri wa Afya)
8. Mhe. Ussi Yahya Haji
9. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
10. Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma)
11. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
12. Mhe. Suleiman Makame Ali
13. Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda
14. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
15. Mhe. Rashid Makame Shamsi
16. Mhe. Bi Chum Kombo Khamis (Naibu Waziri wa Habari)
17. Mhe. Mussa Ali Mussa
18. Mhe. Miraji Khamis Mussa

Waheshimiwa Wajumbe, tunapenda kukushukuruni sana kwa michango yote ambayo mmetuchangia katika bajeti yetu hii. Tunaamini ni kuleta ufanisi kwa sekta yetu ya elimu. Mhe. Naibu Spika, michango kwa kweli ni mingi sana na pia nina wasi wasi kwamba huo muda wa saa moja inawezekana nisimalize. Lakini niseme kwamba kwa yale ambayo tutakuwa tumeyajibu na mengine sio kama hayajajibiwa kama itatokezea muda haukutosha majibu yote

yapo na yote ningeomba sana yaingie katika *Hansard* yetu. Nia na madhumuni yetu ni kwamba kujibu kila hoja ya Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya hoja zimejirejea ina maana sio lazima kumtaja kila Mheshimiwa fulani alisema, nitataja hoja kwa ujumla wake kama ambavyo imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wamechangia katika maeneo makuu hasa ambayo waliyochangia ni katika masuala mazima ya upungufu wa Walimu, suala zima la Vyuo vya Amali ikiwemo Daya na Makunduchi. Waheshimiwa Wajumbe tunajua kwa nini mnaumwa na suala hili, na sio kama mnaumwa nyinyi peke yenu tu lakini serikali nzima inaumwa na suala zima la vyuo hivi vya amali. Tunasema kwamba kukosea njia ndio kujua njia. Tunapokosea katika kuchagua labda wale washauri elekezi ina maana mambo mengi yanakuwa yanafeli. Hilo ndilo ambalo limetukwaza sisi Wizara lakini na serikali kwa ujumla wake. Kwa hilo Waheshimiwa tunakuombeni sana mfahamu kwamba uchungu ambao mnauhisi nyinyi ndio uchungu ambao Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inaumwa sana kuona kwamba tunakopa fedha kwa nguvu za jasho la wananchi lakini tunakwama kutokana tu na kuchagua watu ambao sio sahihi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kukosea njia ndio kujua njia. Muungwana anapokosea njia ina maana anaelekea katika njia sahihi. Kwa hiyo, kwa hili tumejifunza na kupitia kelele zenu waheshimiwa, haina maana kwamba kelele kwa maana ya kelele, lakini kupitia kutugomba kwenu basi nalo hili nalo tumelipokea vizuri sana na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tuombe makosa kama haya yasijitokeze tena katika majenzi mengi ambayo yatakuwa yanaendelea. Tunakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa suala kama hili kulipigia kelele.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa ambayo mengine tayari Mhe. Naibu Waziri ameweza kuyajibu suala zima la walimu wa sayansi na vile vile walimu kutoka Nigeria. Kwa kweli suala hili Mhe. Naibu Waziri tayari ameshalijibu, lakini tokea juzi tulikuwa tuna wakati mgumu sana kupokea simu kutoka kwa waandishi mbali mbali kutaka kujua suala hili. Kumbe kuna masuala mengine ni propaganda ndani ya mitandao ambayo inakuja. Mitandao mingi imeandika kwamba Zanzibar inaajiri walimu zaidi ya 300 kutoka Serikali ya Nigeria, kwa kweli sio jambo ambalo ni sahihi. Tunaomba sana kwa herufi kubwa “MITANDAO JAMANI TUITUMIENI VIZURI SANA” vyenginevyo itakuwa inapotosha wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la walimu wanaojitolea, vile vile nalo limetolewa ufafanuzi na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu. Madarasa ya watu wazima yametolewa ufafanuzi. Uvujaji wa majengo, tunafahamu na tumepokea. Suala la nafasi za walimu ambao wanatarajia kustaafu. Nalo hili vile vile serikali inalifahamu na tayari inalifanyia kazi suala hili. Madrasa na Vyuo vya Qur-an, Ubora wa Elimu, Sera ya Elimu, Masuala ya Malimbikizo, Ubora wa Majengo yanayojengwa kwa nguvu za wananchi, Ubovu wa vyoo maskulini na ubovu wa majengo yaliyozeeka. Suala la Dakhalia, *Tuition* na masuala mengineyo, masuala haya yote yamezungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi ndani ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kujibu baadhi, nitajibu yote *inshaallah* kwa uwezo wa Allah muda ambapo utakuwa unaruhusu. Mhe. Naibu Spika, waheshimiwa akiwemo Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf pamoja na Kamati ya Ustawi, ilitoa ushauri juu ya suala zima la mitaala ya ngazi ya Elimu ya Maandalizi na Msingi.

Mhe. Naibu Spika, suala hii wizara imelipokea na *inshaallah* kuanzia mwezi wa Juni kwa mwaka huu 2018 utaratibu wa kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kupitia mtaala wa elimu ya ngazi ya maandalizi yaani tokea mwaka 2007 utaanza na baada ya hapo utaratibu utaendelea kupitia mtaala wa elimu ya msingi ambao nao uliandikwa mwaka 2009. Waheshimiwa ushauri huu mlioutoa ni mzuri sana na tunaamini kwa ushauri huu na kazi hii ikifanyika basi kama hivyo tunasema kwamba kila kinataka msingi. Kwa hiyio, elimu ya maandalizi na msingi ikiwa imejengwa vizuri tunaamini kwamba hata juu itakapokuwa imenyanyuka kama ni nyumba itakuwa nayo ni katika hali nzuri. Kwa hiyo, kwa hapa *inshaallah* tutalifanyia kazi suala hili na tayari tunaahidi kwamba litafanyiwa kazi kuanzia mwezi wa Juni tutaanza kupitia hiyo mitaala.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la changamoto ya vyoo ndani ya maskuli yetu. Ni kweli tunakiri kwamba kuna tatizo kubwa la vyoo ndani ya maskuli na hasa zile skuli ambazo ni za zamani ambazo walisema wazee wetu mpaka na sisi tukazisoma baadhi ya skuli hizo. Skuli zimezeeka ina maana hata zikizeeka na miundombinu ya vyoo ina maana inazeeka.

Vile vile skuli hizi zilivyojengwa hapo nyuma ilikuwa zinatumiwa na wanafunzi wachache, lakini sasa hivi *Alhamdulillah* tunajitahidi sana katika kuuendeleza Umma wa Muhammad *(SAW),* kila uchao tunajitahidi kufanya hii kazi, kwa hiyo tunapofanya hii kazi mambo mengi nayo yanabadilika. Kuongezeka kwetu sana ina maana hata ile miundombinu iliyojengwa kwa idadi maalum ya watu wakati ule nayo imekuwa imeathiriwa kutokana na wingi wa watu walivyo sasa.

Mhe. Naibu Spika, licha ya hayo wizara inafanya hatua kwa hatua katika kujenga vyoo hivi na kwa mwaka huu wa fedha wizara imekamilisha ujenzi wa vyoo 43 na itajenga vyoo vyengine 30 katika Skuli za Unguja Ukuu, Mchangani, Koani na Mwanakwerekwe “G” hatuwezi kuacha changamoto ya vyoo na ikaendelea kila mwaka ili kujenga mazingira mazuri ya skuli zetu. Aidha, wizara inaendelea kushirikiana na Wahisani wakiwemo *UNICEF* na *Milele Zanzibar Foundation* katika kutatua changamoto hii ya vyoo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika hili tuwashukuru sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa katika Mikoa yao husika, kwa mfano katika Mkoa wa Mjini wa Magharibi Mhe. Mkuu wa Mkoa ameweza kusaidia sana katika ujenzi wa vyoo katika Skuli ya Mwanakwerekwe “E” tunamshukuru sana. Vile vile baadhi ya Waheshimiwa wapo ambao wanasaidia katika ujenzi wa vyoo ndani ya majimbo yao.

Vile vile tumshukuru sana Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu mpendwa Mhe. Samia Suluhu Hassan anasaidia sana katika hatua hii ya ujenzi wa vyoo na analeta mpaka watu kuja kusaidia katika ujenzi wa vyoo. Kwa kweli ni hatua kubwa sana na kwa hili tumeanza vizuri Unguja na Pemba yake na *inshaallah* kazi hiyo itaendelea vizuri sana,

tunamshukuru sana. Lakini vile vile na wadau wengine watakapokuwa wapo tayari basi wanakaribishwa sana katika kutatua tatizo hili, hasa mtu katika ile skuli ambayo yeye amesoma si vibaya akaona anatoa mchango wake katika kuweka miundombinu mizuri ndani ya ile skuli ambayo amesoma akiwa na yeye ni *alumni* wa ile skuli.

Mhe. Naibu Spika, suala la Ugatuzi kwamba wamepatiwa bilioni 55. Mhe. Shehe Hamad Mattar alikuwa anauliza je, kweli tumejipanga vipi. Tumtoe wasi wasi mheshimiwa juu ya suala hili kama ni kweli ugatuzi bado ni mpya, changamoto zinaweza kutokezea kwa sababu wanaofanya kazi ni binaadam. Lakini serikali juu ya hili imejipanga vizuri sana kwa mashirikiano baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kule ambapo kunagatuliwa katika Wizara ya Mhe. Haji Omar Kheri, muheshimiwa ambaye namuamini sana katika kusimamia vyema majukumu ya kazi. Kwa hiyo, ni kusema kwamba fedha hizi zitasimamiwa vizuri sana kupitia halmashauri zetu. Lakini vile vile Wizara ya Elimu imeweza kugatua baadhi ya Maafisa wake ambao walikuwa wanasimamia masuala haya, kwa hiyo nao watakwenda kusaidia katika kuongeza nguvu katika kusimamia masuala haya. Tunaamini na tuombe hivyo kwamba changamoto hiyo isitokezee na fedha zitatumika vizuri sana.

Vile vile Mhe. Shehe Hamad Mattar alitaka kujua suala zima la skuli za binafsi na hili sio peke yake hata baadhi ya waheshimiwa wengine pia waliuliza suala hili kwamba skuli za binafsi kuwachuja wanafunzi na kuwatoa madarasani, nadhani hata Mhe. Ali Suleiman Ali pia alilizungumza suala hilo. Kuwatoa madarasani wasiendelee na masomo yao eti tu kwa kisingizio kwamba wamefeli.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli suala hili hata sisi wizara linatuumiza sana na tokea mwaka juzi tulianza kugombana na baadhi ya skuli za binafsi kwa kuwatoa wanafunzi na zipo baadhi ya skuli tulikaribia kuzifunga kwamba kama hawatarejesha wanafunzi. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba baada ya kuchukua hatua hiyo tulizungumza nao skuli za binafsi na walikubali na waliwarejesha wanafunzi hao. Lakini endapo kama itatokezea kwamba kuna skuli ambayo bado inafanya tatizo hili tunakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi basi tutaarifiane, kuna masuala mengine tusisubiri mpaka tuje katika kikao tutakuwa tayari tumeshaharibikiwa. Kama kuna jambo limetokezea milango ya Wizara ya Elimu ipo wazi, sisi ni wenzenu tumewekwa pale kwa ajili ya kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Katika kusimamia Ilani ya Chama cha Mpinduzi ni wajibu wetu kusimamia kila changamoto ambayo inatokezea ya kielimu. Tunakuombeni sana zinazopotokezea changamoto kama hizi tuleteeni taarifa ili tuweze kuzifanyia kazi kwa haraka zaidi.

Vile vile mheshimiwa alitaka kujua kuhusu dakhalia zinazopatiwa msaada wa chakula na huduma. Dakhalia hizo kwa sasa tulizonazo ni Dakhalia ya Fidel-Castro, Chasasa ama Utaani kwa sababu zipo pamoja zile skuli. Vile vile CCK-Kiuyu, Mazizini CCK ya Wanawake ambayo hii nayo ilikuwa imefungwa kwa muda tulikuwa tunaifanyia ukarabati, lakini sasa hivi ndani ya mwaka huu tunatarajia nayo itaweza kuanza kazi zake vizuri kama tulivyoeleza katika kitabu chetu cha bajeti namna tunavyofanya ukarabati wa dakhalia hii.

Vile vile Dakhalia ya Kengeja Ufundi na Dakhalia ya Mohammed Juma Pindua ambazo zinahudumia wanafunzi wa sekondari. Aidha, kwa sasa serikali ina mpango wa kujenga dakhalia

katika kila eilaya zetu ili tuwe na skuli moja ya mfano na dakhalia ya mfano ambayo itaweza kuwaweka vijana wetu pamoja katika kupata masomo yao.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali ametoa tahadhari kwamba madarasa ambayo yanajengwa kwa nguvu za wananchi tuweze kuyasimamia vizuri ili ubora wake uweze kupatikana. Hili ni kweli na wizara tayari inaandaa muongozo maalum katika kuwasaidia wananchi katika ujenzi wa madarasa. Aidha, wizara kwa kutumia wahandisi wake inafuatilia kwa karibu ujenzi na kutoa ushauri wa kuimarisha ujenzi wa madarasa hayo. Kabla ya kukamilisha majengo hayo wizara huwa inakagua ujenzi husika na inapoonekana ubora wa jengo hauridhishi tunafanya marekebisho kabla ya kuyakamilisha. Wizara imefanya hivyo katika skuli mbali mbali zikiwemo Skuli ya Kandwi, Skuli ya Mgambo, Skuli ya Mwerapongwe, Skuli ya Fuoni Kibondeni, Skuli ya Mangapwani, Skuli ya Chunga pamoja na Skuli ya Maandalizi ya Binguni, tuligundua kasoro na tukaweza kuzirekebisha kabla ya majenzi hayo hayajakamilika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman Sarahan Said alitaka kujua wanafunzi waliokuwepo nje ya mfumo wa elimu wameandaliwa mikakati gani ya kuwarudisha skuli. Ningependa kumjibu kama ifuatavyo juu ya suala hili. Mkakati wa wizara ni kuwahamasisha wananchi kusaidia kusimamia watoto wao katika kupata elimu na umuhimu wa elimu katika maisha kwa jamii na taifa kwa jumla. Hali hii itasaidia sana katika kuwarejesha watoto wetu maskulini. Hili linafanyika kwa mashirikiano makubwa na jamii na Kamati za Skuli katika kuhakikisha inapunguza watoto walio nje ya skuli.

Mhe. Naibu Spika, pia wizara kupitia Programu ya Elimu Mbadala inawapokea watoto hao na kuwapatia elimu. Wizara itawasilisha matokeo ya utafiti wa watoto waliokuwepo nje ya mfumo wa elimu kwa jamii katika Wilaya zetu za Unguja na Pemba. Mpango wa kuwasilisha ripoti hiyo ukikamilika utaanza mwezi wa Juni mwaka huu *inshaallah*. Katika hili tuombe sana jamii kwa sababu mtoto ni jamii nzima. Tuombe sana wazazi kushirikiana katika kusimamia kuona kwamba watoto wetu wanarudi katika mfumo mzima wa elimu. Mtoto unaweza kumpangia kusoma lakini kama mzazi hujamsimamia vizuri sidhani kama mtoto huyo ataweza kusoma, lakini tukishirikiana kwa pamoja basi suala hilo nalo litaweza kukaa vizuri.
Mhe. Naibu Spika, vile vile mheshimiwa alitaka kujua ufundishaji wa maiti katika Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* kwa sababu tulieleza kwamba kile chumba cha maiti tayari kimekamilika cha *Cadaver* ambacho kipo katika Skuli ya Afya ya Mbweni. Alitaka kujua kwamba je, maiti hizo zimeshaanza kutumika ama vipi. Utaratibu wa kufanya mafunzo kwa kutumia maiti yameshaanza na awamu ya mwanzo ya wanafunzi wameshahitimu. Maiti hizi hazitoki Zanzibar kamwe tusiwe na wasi wasi wa hili, maiti zinazotumika tunazipata Hospitali ya Muhimbi Tanzania Bara kwa makubaliano na maandiko maalum, hatuchukui maiti zetu. Tunaomba sana wananchi wetu watuelewe juu ya hili. Vijana wetu wanajifunza wanapata ile *practical* halisi.

Mhe. Naibu Spika, mheshimiwa anataka kujua uwepo wa Waratibu wa *NECTA* ndani ya Zanzibar. Mratibu wa *NECTA* tunae ndani ya Zanzibar ambaye ni Bwana Kassim Abass na pia *NECTA* ina ofisi katika jengo la Bima Mpirani pale Maisara ghorofa ya pili.

Mhe. Abdalla Ali Kombo alitaka kujua nyumba ya Makunduchi je, ile nyumba ni ya serikali au ni ya mtu binafsi. Ile nyumba ni ya serikali, mheshimiwa naona kidogo anazungumza lakini

naamini atakuwa anasikia jawabu yake. Ile nyumba ambayo umeulizia mheshimiwa ni nyumba ya serikali na nyumba ile ipo chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto, kwa hivyo Mheshimiwa usiwe na wasi wasi nyumba bado ipo na inaendelea na ujenzi wake bado haujakamilika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile alitaka kujua ubovu wa paa katika Skuli ya Madungu na skuli nyenginezo. Kwa upande wa Skuli ya Madungu ukarabati wa jengo lile tayari umeshaanza kwa kupitia mkandarasi ambaye alijenga skuli ile mwanzo Kampuni ya Rans na ukarabati ule utakuja kumalizika mwezi wa Agosti mwaka huu.

Waheshimiwa nikuombeni sana kweli tunaumwa na majengo sote lakini kwa hii hapa tayari imeshaanza ukarabati na tunaomba kwa wale ambao mtakwenda Pemba basi ni vizuri mkapita mkaweza kuhakikisha hili jambo kama ni kweli au la. Lakini ukarabati tayari umeshaanza wa majengo hayo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu alitaka kujua vigezo vya mikopo ya elimu ya juu. Mheshimiwa Mwakilishi nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona kila mwenye sifa ya kujiunga na elimu ya juu anapatiwa mkopo. Serikali huongeza bajeti kila mwaka ili kuona kwamba vijana wake wanapata mikopo na fursa ya kuweza kujiendeleza na elimu ya juu. Kwa mfano, mwaka 2016 serikali yetu ilitenga bilioni 6.3 lakini kwa mwaka 2018 tunaona kwamba serikali yetu ilitenga bilioni 10.2. Hii yote ni katika kuona kwamba fedha hizi ziongezeke ili kuona vijana wetu wengi wanapata nafasi zaidi ya kusoma. Tumeshuhudia mwaka huu vijana wengi sana wamepata nafasi ya kupata mkopo na kuendelea na masomo yao.

Lakini suala zima ambalo linazingatiwa hapa ni kwamba ili mikopo iweze kupatikana fani zinawekwa za kipaumbele na Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanyiwa tathmini kila miaka mitano. Vigezo vyengine ambavyo vinatumika ni fani za kipaumbele ambazo zinatolewa na Tume kama nilivyoeleza awali, kwa mfano fani ya mafuta na gesi, walimu wa sayansi, madaktari na wahandisi, hizo ndio fani ambazo zinapewa kipaumbele sana. Lakini vile vile vigezo vinavyotumiwa ni ufaulu wa wanafunzi tunaliangalia sana, umri wa muombaji, jinsia yake, awe Mzanzibari na uwezo wa fedha wa bajeti uliopo. Vigezo hivi tunaviangalia ili kuona namna gani tunaweza kutoa mikopo kwa vijana wetu. Kama umri mtu umempita ina maana itakuwa kwa kweli hapo kapitwa. Lakini vile vile jinsia kwa kweli tunaangalia sana jinsia ya wanawake kupewa kipaumbele hasa wale wa sayansi katika kupata mikopo. Hili kweli wanawake wengi wanapata nafasi ya kupata mikopo.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf alitaka kujua suala zima la madawati limefikia wapi. Tunaamini hichi ni kilio cha Waheshimiwa Wawakilishi wengi wametaka kujua madawati tumechangia lakini hatujayaona. Kwa kweli fedha zetu hazijapotea na mimi nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Madawati ambayo Mhe. Rais ameiunda nalifahamu vizuri sana suala hili.

Mhe. Naibu Spika, fedha tumezichanga kweli tumezipata *Alhamdulillah Rabil Alamiyn*, lakini tunafahamu utaratibu wa mambo yetu kwamba lazima tutangaze tenda na hili ambalo ndio limefanyika. Katika kufanyika utaratibu wa ununuzi wa madawati umefanyika nchini China na kwa sasa wizara imetiliana saini mkataba na Kampuni ya *Guangzhou Everpretty* kutoka China

kwa ununuzi wa madawati haya ambayo ni seti ya viti na meza 44,620. Muda wa mkataba huo ni wa miezi minne na utaanzia mwezi wa Juni, 2018. Hivyo, tunatarajia kupokea madawati hayo baada ya muda huo ina maana muda wowote tunatarajia kupokea madawati kutokana na ule muda wa usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini tumeagiza madawati China. Kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wengi mfano Mhe. Bi Panya Ali Abdalla na wengineo wamesema kwa nini tusichongeshe madawati ndani ya nchi yetu. Ni kweli kwamba tunajua Chuo cha Ufundi wanachonga madawati, vile vile JKU na katika Vikosi vyetu nao pia wanachonga. Serikali imefikiria kufanya hivyo ama Kamati chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Haroun Ali Suleiman imeona ni vyema kununua madawati kutoka nchi ya China kutokana na urahisi wa bei ya madawati ukilinganisha na gharama za ununuzi kwa hapa nchini kwetu. (*Makofi*)

Aidha, kabla ya kufanya kazi hii maamuzi ya timu ya wataalam ilitembelea viwanda mbali mbali katika nchi ya China kutafiti ubora na gharama za madawati katika viwanda hivyo.

Kwa hiyo, waheshimiwa juu ya suala hili hatukukurupuka tuliumiza akili sana na tulijiuliza kwa nini tusifanye madawati yetu hapa, lakini unakuta kwamba ile gharama ambayo tuliyokuwa tunaikimbia dawati moja shilingi 300,000/= kwa hapa kwetu, tunakubali kwamba kweli ubora wake ni mzuri, lakini na huko China nako tumekwenda na wataalum ambao wanafanya kazi hizo katika chuo chetu cha Karume. Kwa hivyo katika kukagua tumekagua ubora wa dawati ambalo litakuja hapa na tunaamini kwamba dawati ambalo litakuja hapa litakuwa ni imara na litadumu na vijana wetu watayatunza vizuri sana. Kwa hivyo, waheshimiwa fedha zetu hazijapotea zipo na wakati wowote tutarajie kwamba madawati haya tutakapokuwa tunayasambaza basi itakuwa ni harambee kubwa sana na kila mmoja kwa siku hiyo nadhani atakuwa anajisikia vizuri sana.

Vile vile mheshimiwa mmoja alitaka kujua idadi hasa ya madawati nadhani Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Aidha, jumla ya mahitajio ya vikalio vyote kwa skuli za Unguja na Pemba ni seti ya viti 18,844 kwa skuli za sekondari, maana tukisema seti ya viti ina maana kiti na meza yake, na madawati 29,140 ya wanafunzi watatu watatu kwa skuli za msingi Unguja na Pemba. Hata hivyo, makisio haya na kwa mujibu wa takwimu yetu ambayo tulimalizia kwa mwaka pale 2017 tukiri kwamba baada ya kuandikisha wanafunzi ndani ya mwaka huu wanafunzi wameongezeka sana. Kwa hivyo, ile takwimu hasa ambayo sasa hivi itakuwa imeongezeka ina maana kuna ongezeka ambalo limeongezeka, lakini mpaka kufikia mwaka 2017 ilikuwa tunahitaji madawati viti na meza idadi hiyo hapo ambayo nimeitaja.

Tunafanya hivyo kwa sababu tunaona kwamba kwa upande wa sekondari tunataka kuondosha ile kutumia madawati ya watu watatuwatatu kwa sababu yanatukwaza sana wakati wa mitihani inakuwa ni usumbufu darasa linakuwa linatumika kwa wanafunzi wachache sana. Lakini yatakapokuwa madawati yetu haya mapya viti na meza vitakwenda kwa wanafunzi wa sekondari na madawati ya watu watatu watatu yatatumika kwa wanafunzi wa msingi. Sote tunafahamu kwamba wale watoto ni wadogo, wanakuwa watundu sana wanaweza kufanya vyovyote ambavyo wanaweza kufanya. Lakini lile deski likiwa zito si rahisi kwa watoto wadogo kuweza kulivunja. Kwa hivyo, huo ndio utaratibu ambao tutaweza kuutumia.

Mhe. Simai Mohammed Said alitaka kujua kuhusiana na kutokujua kusoma Kiingereza, Math pamoja na *Geography* hali sio nzuri juu ya suala hili. Mheshimiwa ni kwamba kupitia mradi wa *ZUSP* kuna kipengele cha kujifunza somo la Math ambamo humo mna Hesabati na Kiingereza ambapo walimu wanapatiwa mafunzo ya masomo hayo ili kupata mbinu bora na kuongeza taaluma zao. Idara inaandaa mashindano ya insha na midahalo kuimarisha vipaji na uelewa wa masomo hayo. Idara ikishirikiana na wadau mbali mbali kama Kituo cha Huduma za Sheria, Jumuiya ya Afrika Mashariki na skuli ya Feza Zanzibar tunawashirikisha katika uandishi wa insha ili kuona kwamba vijana wetu wanakuwa imara zaidi katika masuala mazima ya lugha. Na tukubali tukitaka tusitake ni kwamba sisi lugha yetu ya kwanza ni Kiswahili kwa hiyo hata mtoto anapokuwa yupo skuli ukimsomesha Kiingereza akirudi nyumbani wazazi wake wote wanaongea lugha ya Kiswahili.

Kwa hivyo, unakuta ule muda wa mwanafunzi kupata mazoezi ya wakati mwingi unakuwa ni mdogo, lakini ni vizuri tukajenga utamaduni kwamba mtoto akirudi skuli ameshasoma Kiingereza basi akija na nyumbani hivyo hivyo tujaribu kumzungumzisha, hili lengo ambalo tunataka lifikiwe liweze kufikiwa. Lakini kama mtoto muda wa masaa matano yupo skuli, akija nyumbani muda wa masaa mengi zaidi anaongea Kiswahili muda wote kwa kweli kidogo inakuwa hajengeki vizuri sana. Kwa hivyo, niombe sana wananchi tuwe na mwamko huo tuwashajihishe watoto wetu majumbani tuwazungumzishe ile lugha ya Kiingereza ili waweze kupata mazoezi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mheshimiwa alitaka kujua kuhusiana na suala zima la uhaba wa vifaa katika vituo vya amali nadhani Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) kama itakuwa sijakosea. Kwa mfano katika Kituo cha Elimu Mbadala Wingwi, Mtemani alisema kwamba kuna uhaba mkubwa wa vifaa katika kituo hicho. Ni kweli kwamba kuna upungufu wa vifaa lakini wizara tayari imechukua juhudi ya kupunguza tatizo hilo kwa kukipatia kituo hicho vifaa vya fani ikiwemo vyarahani, kompyuta, mashine ya fotokopi, vifaa vya upishi pamoja na vifaa vya umeme. Pia hivi karibuni wizara yetu imepeleka vitabu vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya walimu na wanafunzi katika kituo hicho cha Wingwi.

Vile vile Mhe. Mwakilishi baadhi yao wengi lakini Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alikuwa kabeba bendera hii kutaka kujua kwa nini madarasa ya watu wazima yanaendelea hadi hii leo hayeshi, tuko miaka 54 ya Mapinduzi lakini bado madarasa haya yanaendelea. Kuendelea kuwepo kwa madarasa ya elimu ya watu wazima kumechangiwa na sababu mbali mbali zikiwemo kuwepo kwa vijiji ambavyo vilikuwa mbali na skuli ambako kumepelekea wananchi wa vijiji hivyo kutokuandikishwa katika skuli kwa umri husika. Kwa hiyo, ina maana sababu hiyo imepelekea kwamba kwa watu wale mpaka wanakuwa hawajui kusoma wala kuandika.

Lakini vile vile utoro wa wanafunzi katika maskuli yetu hasa wa ngazi ya elimu ya msingi kumepelekea kufikia umri mkubwa wakiwa vijana wetu hawajui kusoma wala kuandika na hivyo mtoto akishakujiona ameshakua mkubwa anajiona mimi tena kwenda kusoma na watoto wenziwe hawezi kwa hivyo lazima aende akajiunge na elimu hii ya watu wazima.

Lakini vile vile mwamko mdogo wa elimu kwa baadhi ya wananchi kutokuandikisha watoto wao katika elimu ya msingi na katika umri sahihi kumepelekea kufikia idadi hiyo ya vijana ama

watoto ambao hawajui kusoma wala kuandika na hatimae vijana hao kujiunga na madarasa ya elimu ya watu wazima.

Hata hivyo, serikali yetu tukufu inahitaji kupunguza tatizo hilo la watu wasiojua kusoma na kuandika na kuhesabu kwa asilimia 30 miaka ya 1970 hali asilimia 84 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Kwa hiyo, ni kusema kwamba serikali yetu inafanya kila jitihada ya kuona kwamba wananchi wake wengi wanajua kusoma na kuandika.

Kwa hiyo kwa sababu hizo ambazo zimetajwa na nyenginezo inapelekea kuona kwamba madarasa haya bado yataendelea kuwepo. Tusijione tunakaa mjini skuli zimejaa kila pahala tukadhani kwamba huko vijijini hali ni kama hiyo. Skuli sasa hivi zipo kote lakini bado mwamko wa baadhi ya watu ni mdogo sana kwa hiyo hii inapelekea hali kama hiyo kutokezea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said vile vile alitaka kujua kwamba serikali suala la *tuition* inasemaje. Serikali juu ya suala la *tuition* ilitoa muongozo wa matumizi sahihi ya *tuition* kwamba *tuition* mwisho iwe ni saa mbili tu, lakini *tuition* hii kama *tuition* haina maana kama itakuwa ni *tuition* tu bali lazima isajiliwe na Kituo cha Elimu Mbadala na Watu Wazima. Kwa hiyo, *tuition* kama ili iwepo ina maana lazima wizara iwe inatambua pahala gani kuna *tuition* na sifa zake.

Mhe. Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga alitaka kujua kwamba je, katika jimbo lake yeye madarasa haya yapo ama hayapo. Katika Jimbo la Chonga darasa hakuna lakini katika majimbo mengine madarasa yapo. Lakini Waheshimiwa Wawakilishi tuwekeni kipaumbele katika kuona kwamba suala zima la elimu ni muhimu sana ndani ya majimbo yetu, tuangalie elimu kuanzia maandalizi, msingi, sekondari ya juu mpaka madarasa ya kisomo kwa sababu wananchi wetu wanakuwa wapo ambao hawajui kusoma na kuandika lakini kwa sababu hatujawatafuta tunaona kwamba hatujui. Kwa hiyo, kwa hili tunaomba sana tushirikiane ili kuona kwamba wananchi wetu wanaepukana na tatizo la kutokujua kusoma na kuandika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo na yeye juu ya suala hili hili alisema kwamba kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya elimu ya watu wazima. Je, kwake yeye zipo na wanafaidika vipi na fedha hizo. Juu ya hili tuseme kwamba zinapotajwa fedha haina maana kwamba pengine kila mtu kwa namna moja au nyengine atakuwa anapewa pesa mkononi, lakini tunapopeleka vifaa kwa mfano tunapeleka penseli, mabuku ya kuandikia na vifaa vyengine vya kusomeshea na kusomea inakuwa tayari fedha zile zimeweza kutumika. Kwa hiyo, kinachofanyika ni hicho kwa kupeleka vifaa. Hata huko kwako Mhe. Bahati ni kwamba tunanunua vifaa na wale wanakisomo wanapata kusomea.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla alitaka kutoa kipaumbele zaidi katika somo la Kiingereza kwamba lipewe kipaumbele. Mheshimiwa somo la Kiingereza linasomeshwa katika madarasa ya maandalizi, msingi na sekondari na yote tunayafanya haya kwa kujua umuhimu wa lugha. Ni kweli tuna lugha yetu ni utamaduni wetu lakini haina maana kwamba tujibane tusiweze kujua lugha nyenginezo, lugha ya Kiingereza ni lugha ya kimataifa na ni wajibu wa vijana wetu na wao kuweza kujua.

Kwa sababu tunamjenga mtoto katika mazingira yote yote suala la kitaifa lakini vile vile kimataifa. Kwa hiyo, tunaamini kwamba akeshakuwa na msingi mzuri wa lugha ina maana itaweza kumsaidia kupata kazi ama kujiajiri yeye mwenyewe hata katika mataifa mengine. Na ushahidi wa hili tunao vijana wengi ambao wanafanya kazi ndani ya mataifa mengine ni Wazanzibari lugha yao ya kwanza ni Kiswahili lakini wanafanya vizuri sana katika lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, hili wizara inalijua na kipaumbele hicho kipo.

Suala la vifaa ambavyo vimegaiwa vitabu Mhe. Zaina Abdalla Salum aliuliza na alisema kwamba yeye atazuia. Mheshimiwa kwa hili nikuombe sana kwamba najua nia yako ni thabiti lakini serikali yetu tukufu haibagui mtu wa aina yeyote. Serikali yetu ni sikivu sana na inapenda kuona kwamba inatoa huduma kwa wananchi wake wote bila ya kujali jinsia ya mtu, umri wa mtu ama kabila gani ama ana wajihi gani na lolote jenginelo. Kwa hiyo, serikali yetu haibagui. Kwa hiyo, mheshimiwa ni kwamba vitabu vya nukta nundu vimegaiwa katika skuli zote zenye uhitaji wa vitabu hivyo na vitabu vya darasa la tano na darasa la sita vimepelekwa katika skuli ya Micheweni, Ole, Furaha, Minungwini, Mchangamdogo na skuli nyenginezo.

Lakini kwa upande wa Unguja Skuli ya Jambiani, Kiswandui, Moga pia nazo zimefaidika na kupata vitabu hivyo. Kwa hiyo, mheshimiwa tunapeleka inawezekana pengine kwamba wahitaji ni wengi sana lakini vifaa vinakwenda na tunakuomba sana kwamba tuwapatie fedha hizi ili ziweze kuwasaidia vijana wetu hawa ambao wana mahitaji maalum nao waweze kupata nafasi kama vijana wengine ambavyo wanapata.

Mhe. Mohamed Said Mohamed alikuwa anahoji kwa nini vyuo vinafungwa kutokana na kutokidhi masharti ya usajili wa taasisi zinazohusika na usajili kama vile *NACTE, TCU* ama *VTA*.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kumetangazwa kwamba baadhi ya vyuo vimefungiwa, lakini kuna vyuo vilivyotajwa hasa vile vyuo vya serikali ni kwamba vile vyuo vimefutiwa usajili kutokana na kwamba vyuo vile tayari vimebadilisha hadhi kutoka *NACTE* sasa vipo chini ya *TCU*. Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi sasa kimekuwa ni sehemu Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA),* Chuo cha Afya Mbweni ni sehemu ya *SUZA,* vile vile ya Chuo cha Chwaka nacho ni sehemu ya *SUZA.* Kwa hiyo, moja kwa moja vyuo hivi sasa vimekuwa ni skuli ndani ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Kwa hiyo, usajili wake upo chini ya *TCU* mamlaka ambayo inasimamia vyuo vikuu nchi kwetu. Ina maana havijafutwa kwa maana ya vyuo havipo lakini usajili wake sasa umeondoka katika *NACTE*.

Mhe. Naibu Spika, kwa vyuo vyengine ambavyo labda vimefutiwa usajili ni kwamba tatizo liliopo chuo kwa mfano kinaomba usajili kusomesha kozi tatu, lakini ndani yake anasomesha kozi kumi, ina maana kozi saba hizi hajazisajili. Kwa hiyo, imefungiwa zile kozi ambazo hazijasajiliwa na *NACTE,* lakini zile kozi nyengine ambazo bado zimesajiliwa ina maana zitakuwa zinaendelea kama kawaida. Najua suala hii tuwaombe sana vijana wetu wanapojiunga na vyuo tuwe na tahadhari sana kuona kwamba je, chuo ambacho anakwenda kujiunga kimesajiliwa ipasavyo. Kwa sababu baadhi ya vijana ama ndio sisi wazazi anakwenda kuona chuo kimebandikwa bango au *college* anakwenda kujiunga lakini unakuta chuo kile hakina usajili ambao unatambulika. Inakuwa hapa ni kuwapotezea muda vijana wetu.

Tuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe tuwe walimu wa kuwaelimisha vijana wetu juu ya suala hili kwamba wachague vyuo ambavyo vimesajiliwa na vinatambulikana rasmi ndani ya nchi yetu ya Tanzania na sio tu kwamba chuo mtu kaamka asubuhi akasema nataka kuweka na mimi skuli ama chuo akakodi jengo halafu akabandika tukenda kupeleka vijana wetu.

Suala la walimu tayari limeshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitoa ushauri mzuri sana kwamba tuweze kuangalia *syllabus* zetu, tuangalie walimu wetu, tuangalie mambo mengi. Ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi *inshaallah*.

Mhe. Mussa Ali Mussa alikuwa anauliza wizara inawaangalia vipi walimu wa Vyuo vya Qur-an. Nadhani Mhe. Naibu Waziri suala hili tayari ameshalifafanua ipasavyo. Juu ya suala hili ni kwamba ni vyema niongezee kama Mhe. Naibu Waziri alilisema kwamba suala hili lipo chini ya Ofisi ya Mufti kwa hiyo naamini amesikia maoni ya Waheshimiwa Wawakilishi ambao mnawakilisha wananchi ndani ya majimbo yetu na pengine litatizamwa vizuri sana juu ya suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, Skuli ya Uvinje *inshallah* skuli tutaitembelea kwa sababu sasa hivi tupo katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan lakini vile vile tupo katika kikao cha bajeti kwa maana itakuwa si rahisi kuweza kwenda. Lakini tukimaliza bajeti yetu *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitufikisha na sisi wizara na mimi binafsi yangu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu tutakwenda kutembelea skuli hii ya Uvinje lakini na skuli nyenginezo zote tutakwenda kuzitembelea. Waheshimiwa tunaomba sana mje mtupokee huko Pemba tunataka kuja kuweka kambi maalum tuje kwenye majimbo yenu. Kwa hiyo, tunaomba sana tutakapokuja huko basi mtupokee vizuri sana ili tuone kwamba katika kila jimbo katika skuli zetu tunazitatua changamoto ambazo zipo hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, vile vile waheshimiwa walitaka kujua kuhusiana na suala zima la walimu ambao hawajasomea. Je, wizara tuna utaratibu gani juu ya walimu hawa. Ni kwamba sisi wizara tunatambua kwamba kuna changamoto za walimu ambao hawajasomea na ndio maana tumeanzisha Programu maalum za Elimu Masafa ili kuweza kupata ufumbuzi juu ya changamoto hii ambayo inajitokeza na mafunzo yanatolewa kupitia vituo vya walimu yaani *TC* Unguja na Pemba, walimu wanapatiwa mafunzo ya cheti cha Ualimu daraja la 3B na 3A. Vile vile walimu hawa hushauriwa wajiunge na mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Ualimu baada ya kumaliza hatua hiyo. Tunajua suala hili tunaamini kwamba tutakuwa tunatatua tatizo hili la walimu ambao hawajasomea lakini walimu ambao ingekuwa ni wazoefu sana.

Mhe. Bahati Khamis Kombo vile vile alitwambia Skuli ya Dodo, Mwambe, Shamiani zote zipo katika hali mbaya sana. Tunafahamu kwamba kweli kama tulivyoeleza awali kwamba majengo mengi yameshazeeka. Kwa hiyo, tunajua kwamba skuli nyingi zinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Kwa hiyo, wizara imelipokea na katika skuli hizi mheshimiwa ni kwamba hazihitaji ukarabati mkubwa na hasa ukizingatia kwamba bajeti hii mengine hayatawezekana kufanyika kama ambavyo tutafanya nyenginezo. Lakini kwa zile skuli nyengine ambazo tumezitaja katika kitabu chetu cha bajeti zile ndio tutakazozipa kipaumbele, pale ambapo zitakamilika kama fedha

zitakuwa zimebakia basi tutaangalia na majengo mengine ambayo yanahitaji kupatiwa huduma kama hiyo, likiwemo na jengo la Skuli ya Shaurimoyo kwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Waheshimiwa wengi mlitaka kujua suala zima la Daya na lini ujenzi huo utaendelea. Baada ya matatizo yote ambayo yametokezea nadhani mengi nimeeleza awali tatizo la Mshauri Muelekezi tumejifunza, lakini kuanzia mwezi ujao wa Juni na matatizo haya yamekamilika kwa hiyo tunatarajia kwamba ujenzi utaendelea katika kituo kile cha Daya Mtambwe.

Mhe. Naibu Spika,Waheshimiwa Wajumbe vile vile mlitaka kujua suala zima la kuwafundisha walimu mia mbili kumudu kufundisha madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Mpango huu hauna lengo la kuwaongezea mzigo walimu, lakini lengo ni kuwasaidia walimu hao kumudu kufundisha madarasa hayo ukizingatia changamoto iliyopo ni kubwa kwa hivi sasa na watoto wetu wanataka kusoma. Kwa hiyo, ili tuweze kuwasaidia kusoma ni vyema walimu wetu hawa kuweza kuwasaidia kupata mafunzo maalum na kuweza kumudu kuwasomesha wanafunzi wa madarasa makubwa. Kwa hiyo, ndio maana tunafanya hivyo ili kuona kwamba tunalisaidia hilo suala.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tulishauriwa kuhusiana na suala zima la miundombinu kwa watu wenye mahitaji maalum bado ni changamoto ikiwemo vifaa na wataalam. Mazungumzo gani ambayo yamefanyika. Wizara yetu kupitia Kitengo cha Elimu Mjumuisho ya Stadi za Maisha inaendelea kufanya mazungunzo na wataalam mbali mbali wakiwemo wahisani kuona kwamba masuala haya yanachukuliwa hatua zinazostahiki ili kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kujifunza kwa ufanisi wa hali ya juu.

Kwa upande wa miundombinu wizara inajenga *ramps* katika skuli 50 kwa mwaka 2017 kwa ufadhili wa *UNICEF,* pia inatazamia *ramps* katika skuli 50 nyengine kwa mwaka 2018 kwa ufadhili wa *GPE*. Kwa upande wa vifaa wizara inaendelea kufanya ununuzi wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kadri hali ya fedha inavyorushu.

Katika mwaka 2017 vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 192 vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ufadhili wa *UNICEF* kwa mashirikiano na *GPE*. Kwa upande wa wataalam wizara imewapatia mafunzo ya kutengeneza mashine za kuandikia maandishi ya nutkta nundu pamoja na mashine za kuchapia maandishi hayo wataalam wanne. Pia wataalam wengine wanne wamepata mafunzo ya kutengeneza shime, sikio yaani *eye mole* pamoja na kurekebisha *hearing aids.* Na katika suala zima la hii miundombinu ya watu wenye mahitaji maalum labda tukiri kwamba kwa zile skuli nyingi za zamani kweli miundombinu hii haiko vizuri, lakini ina maana wizara inafanya jitihada ya kuona kwamba tunajenga miundombinu hiyo ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wote ambao wana mahitaji maalum.
Lakini kwa yale majengo mapya ambayo yanajengwa sasa basi suala hilo linazingatiwa vizuri sana na katika skuli zote ambazo zinajengwa kwenye miaka hii ya karibuni suala hilo linazingatiwa sana na miundombinu hiyo inakuwa ipo. Lakini kwa zile skuli ambazo zimeshazeeka na kweli ni changamoto lakini tunafanya kila jitihada kuona kwamba nako kunamalizika.

Vile vile Mhe. Zaina Abdalla Salum alitaka kujua suala zima la wanafunzi wenye uhitaji wa wanafunzi viziwi wanakabiliwa na tatizo kubwa la kutokuwa na wataalam katika fani hiyo. Wizara yetu inalitambua hilo na tunafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuona kwamba jambo hilo nalo linapatiwa ufumbauzi, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya lugha ya alama kwa walimu na wanafunzi ili waweze kujifunza kadri ya uwezo wao. Vile vile katika hili ni kwamba Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)* kuna kozi ile ya diploma elimu mjumuisho ambayo inasomesha kozi maalum kwa ajili ya kuwasaidia vijana ambao wana mahitaji maalum. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba watakapokuwa wanakamilika wanamaliza masomo yao wataweza kusaidia kutatua tatizo hili. Lakini vile vile na vyuo vyenginevyo hata nje ya Zanzibar, Tanzania Bara viko vyuo ambavyo vinasomesha kozi hizi na tunawaomba sana walimu wetu nao wasome ili waweze kuwasaidia vijana wetu.

Mhe Zaina Abdalla Salum vile vile alikuwa na wasi wasi kwamba Skuli ya Mwanakwerekwe ni skuli ya wanafunzi viziwi lakini wananyanyasika. Kama tulivyoeleza awali kwamba serikali yetu haipendi kuona wananchi wake wananyanyasika na katika hili ndio maana tunakuwa tunatoa mafunzo maalum ya lugha za alama kwa walimu ili waweze kuwasaidia vizuri sana wanafunzi wetu hawa. Na kama kunatokea tatizo kama hilo kwamba wanafunzi wananyanyasika Mhe. Zaina tunakuomba sana tuarifiane ili walimu hao tuweze kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria kama ambavyo inasema.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) alitaka kujua kwa nini wale ambao walimaliza Chuo cha Kiislamu hawapati nafasi ya kujiunga na Vyuo Vikuu. Mheshimiwa wanafunzi waliomaliza Chuo cha Kiislamu walikuwa wakijunga na Vyuo Vikuu vilivyopo hapa nchini lakini imeonekana kwamba kuna baadhi ya wanafunzi hufanya udanganyifu katika kujiunga na vyuo hivyo. Kwa hivyo, ili kuondosha hali hii Taasisi ya Kuendeleza Mafunzo ya Ufundi imeanzisha nambari maalum kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo ya aina fulani ili kuthibitisha uhalali wao. Kwa bahati mbaya chuo chetu kipo chini ya Wizara ya Elimu na sio *NACTE* na kwa hivyo wanafunzi hao wamekosa nambari hizo.

Kwa hivi sasa wizara kwa kushirikiana na *NACTE* imeshawapatia nambari baadhi ya wanafunzi na wengine wapo katika mchakato wa kuweza kupatiwa nambari hizo. Kwa hivyo, kwa kila mwanafunzi atakayekuwa na sifa ataweza kupokelewa kuendelea na masomo yake ya Chuo Kikuu.

Vile vile Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) alikuwa anahoji suala zima viashiria vya kurejesha mikopo idadi ya warejeshaji lakini katika shabaha ya utekelezaji imewekwa kiwango cha fedha. Mheshimiwa tunakubaliana na wewe na tumekubaliana na ushauri wako huo ambao umeutoa na tumeupokea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba kwa michangio mingi ambayo imetolewa naona kama nimeweza kuijibu na kama kwa bahati mbaya imetokezea sijajibu labda itakuwa … lakini naamni kwamba nimejibu michango ya waheshimiwa wote kama ambavyo wametoa.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, lakini vile vile niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao ambayo wameitoa na naamini kwamba

waheshimiwa tunakuombeni sana tuaminini kama ambavyo mlivyokuwa mnatuamini toke huko nyuma hadi sasa. Tuaminini sana tuko katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, mtuamini kwamba tumepewa kusimamia sekta ya elimu basi kwa nguvu zote tutaendelea kusimamia sekta hii ili kuweza kumsaidia sana Mhe. Rais wetu ambaye anaumwa na uchungu sana na Sekta ya Elimu pamoja na Afya na nyenginezo ikiwemo maji na barabara.

Waheshimiwa tunajua kwamba nyote ni Wawakilishi wa Majimbo, ndani ya majimbo yetu tuna maskuli, tuna vyuo mbali mbali ambavyo vina changamoto nyingi, tushirikiane kuona kwamba kwa pamoja tunatatua matatizo haya. Maendeleo ya nchi hujengwa na wananchi wenyewe na sisi ndio wananchi wenyewe wa kujenga nchi yetu. Kwa hiyo, waheshimiwa tunakuombeni sana tujengeni nchi yetu kwa mapenzi yote na uzalendo wetu tukikumbuka kwamba sote humu ndani tunasimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Ili ilani yetu iweze kufanya kazi vizuri ni wajibu wetu sisi Waheshimiwa Wawakilishi kuonesha mfano wa kusimamia hili. Kwa hiyo, nikuombeni sana tupitishe bajeti yetu vizuri ili hili liweze kufikiwa na zile ahadi ambazo Mhe. Rais amezitoa, zile ahadi ambazo Serikali yetu ya CCM imeziahidi basi naomba sana tuweze kuzitekeleza kwa pamoja.

Waheshimiwa nia ya serikali ni kuona kwamba elimu inakuwa ndani ya nchi na pale ambapo pana matatizo tuambizane ili mambo yaende vizuri sana. Tunamshukuru sana, sana Mhe. Rais kwa juhudi zake kubwa ambazo anazifanya katika sekta hii ya elimu. Sote ni mashuhuda Mhe. Rais amefuta michango ya maandalizi na msingi lakini tayari na sekondari nazo zimefuata. Juzi tumeona amezindua kitabu chetu hata picha inajionesha hiyo hali. Tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa hili na juhudi zake katika Sekta ya Elimu pamoja na Msaidizi wake Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa nguvu ambazo wanashirikiana na Mhe. Rais.

Lakini vile vile tunawashukuru Mawaziri wote ambao nao wanasimamia sana sekta ya elimu katika sekta zao kwa sababu barabara haijengwi kama hakuna elimu iliyokuwa nzuri, hawezi kupata mtaalam kama hajasomeshwa, hatuwezi kupata mwanasheria kama hajasomeshwa. Kwa hiyo, kila mtaalam lazima asomeshwe. Tuna masuala ya mafuta na gesi sasa inataka wataalam, tunafanya kila jitihada kuona kwamba tunapata *scholarship* mbali mbali ndani na nje ya nchi kuona kwamba vijana wetu wanapata nafasi hizo ili kupata wataalam.

Waheshimiwa tuungane kwa pamoja tusimamie Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini tuone kwamba Mhe. Rais ahadi ambazo amezitaja, ambazo ameahidi anatekeleza lakini tumuunge mkono ili kuona kwamba tunamaliza zote. Changamoto hazishi kwa sababu kila siku tunaendelea kuongezeka, na sisi humu ndani kila mmoja tumekuja humu wengine ana mmoja tumeondoka huyu ameshapata na mwengine, hujui tena wengine huko watamaliza vipi lakini naamni kwamba idadi itaongezeka.

Waheshimiwa tunakushukuruni sana kwa michango yote. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, Ramadhan Kareem. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri ameshatoa hoja wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyokubaliana kwa hoja ambayo ameileta Mhe. Hamza Hassan Juma na kutokana na kwa kweli uzito wa Wizara hii pamoja na kupitia michango mingi ya Waheshimiwa Wajumbe na kwa kutaka kupata majibu kwa ufafanuzi mpana zaidi, Mheshimiwa ambaye amepata wakati mzuri wa kutoa maelezo nahisi kwamba ilikuwa busara nzuri kabisa ya kuachia tuweze kupitisha mafungu siku ya Jumatatu.

Kwa bahati hapa mimi nilikuwa sijui nimekaa hapa sasa wengi wananiandikia vi-*note* nimeshukuru kumbe nilikuwa sijui tuna Maimamu wengi mno hapa. Kwa hiyo, ilikuwa hoja ya kuleta hiyo kwamba tumalize Jumatatu ilikuwa ni ya msingi kabisa kwa sababu tuwaachie Maimamu wakafanye kazi yao nyengine huko mitaani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa leo na *inshaallah* tukijaaliwa tutakutana tena siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi naakhirisha kikao.

(Saa 5:48 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 28/05/2018 saa 3:00 asubuhi)